SUPA JACKPOT
TZS. 1,059,844,733
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

UKURASA 4



**MZEE** auawa kwa kukatwa panga, imani za ushirikina zatajwa kiini




UKURASA 13

Nipashe
Jumamosi Desemba 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581169
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Hujuma malipo wenye vyeti feki

**WAZIRI** abaini tatizo lilipo, atoa angalizo.... *Endelea Uk. 2*



Watawa wa Kanisa Katoliki ambao majina yao hayakupatikana, wakichagua miti ya Krismasi ikiwa ni maandalizi ya sikukuu hiyo ambayo huadhimishwa Desemba 25, kila mwaka, kama walivyokutwa mtaa wa One Way, jijini Dodoma jana . **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

## Wauguzi matatani kwa tuhuma kugoma kumhudumia mjamzito

UKURASA 2

## Mtoto wa umri miaka sita adaiwa kujinyonga

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA, AZAM FC MECHI YA KIBABE UK. 32

**KATUNI** UK. 6



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama akihimiza utekelezaji wa agizo la kuwarejeshea michango waliyochangia katika mifuko ya hifadhi ya jamii watumishi walioondelewa katika utumishi wa umma kwa kughushi vyeti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hujuma malipo michango ya walioondolewa kwa vyeti feki

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imebaini kutotekelezwa kikamilifu maelekezo yake ya kulipwa kwa michango iliyopo kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ya watumishi walioondolewa kwenye orodha ya utumishi kutokana na vyeti feki.

Mnamo Oktoba 27 mwaka huu, serikali ilitoa maelekezo ya namna ya kushughulikia watumishi hao wa umma, ikiwataka waajiri kutoa ushirikiano kwa watumishi walioghushi vyeti pindi wanapofika kwenye ofisi zao kukamilisha taratibu za ulipwaji ikiwa ni pamoja na kuwasilisha nyaraka muhimu kwa ajili ya kulipwa michango yao walioiachanga kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii na kujaza na kutia saini Hati ya Ridhaa (Commitment Bond).

Serikali pia iliwaagiza waajiri wote kuwasiliana na ofisi za mifuko ya hifadhi ya jamii za wilaya na mikoa ili kupata taarifa sahihi za watumishi hao zinazohusiana na kazi hiyo.

Vilevile, serikali iliwataka waajiri kuandaa na kuwasilisha kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii hati ya ridhaa pamoja na nyaraka nyingine kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya mifuko husika.

Serikali pia iliagiza kuandaliwa dawati la msaada ili kufanikisha na kurahisha mchakato wa ulipaji wa michango hiyo ikiwa ni pamoja na ujazaji wa mkataba wa makubaliano (Commitment Bond), pia kuzingatia misingi ya utawala bora ikiwa ni pamoja na kuepuka vitendo vya rushwa wakati wa kazi hiyo.

Hata hivyo, katika taarifa yake jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama alibainisha kuwa licha ya kutoa maelekezo hayo, ofisi yake imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya walengwa wanaohusika na kazi hiyo kuwa baadhi ya waajiri hawatekelezi maelekezo hayo ya serikali kwa ukamilifu.

Alisema shida zaidi imejitokeza katika kutoa ushirikiano katika ujazaji wa Hati ya Ridhaa (Commitment Bond) pamoja na kuchelewesha kuwasilisha vielelezo husika kwa ajili ya kuwawezesha walengwa kurejeshewa michango yao, jambo ambalo linaleta usumbufu kwa walengwa kufuatilia msamaha ambao Rais ameutoa.

"Kwa kuwa nina dhamana ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia masuala ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ninatumia fursa hii kwa mara nyingine kuwaelekeza tena waajiri wote kuhakikisha wanatekeleza ipasavyo maelekezo ya serikali niliyoyatoa mnamo tarehe 27 Oktoba 2022.

"Kupitia ofisi yangu, nimekwishakuunda timu ya kufanya uhakiki na kufuatilia mienendo ya waajiri wote katika kutekeleza maelekezo haya ya serikali. Ninaamini kila mwajiri atatekeleza wajibu wake ipasavyo." aliagiza.

Oktoba 26 mwaka huu, ilitangazwa na serikali kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia kuwa watumishi wote walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti warejeshewe michango yao waliyochangia kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

Watumishi hao ni wale walioondolewa katika utumishi wa umma katika shughuli maalum la uhakiki wa vyeti lililoendeshwa na serikali kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) katika kipindi cha kuanzia Oktoba 2016 hadi Aprili mwaka 2017.

Kufuatia uhakiki huo, watumishi wasiopungua 14,516 walibainika kuwa na vyeti vya kughushi na waliondolewa katika utumishi wa umma.

Kufuatilia maelekezo hayo, Mfuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) utarejesha michango ya wafanyakazi iliyowasilishwa kwenye mfuko hiyo bila kuhusisha michango ya mwajiri.

Marejesho ya michango hiyo yalipangwa kuanza kufanyika kuanzia Novemba Mosi mwaka huu, mtumishi husika akitakiwa kwenda kwa aliyekuwa mwajiri wake akiwa na picha mbili za saizi ya hati ya kusafiria.

Vingine anavyotakiwa kwenda navyo ni nakala ya taarifa za benki ya akaunti iliyo hai na nakala ya Kitambulisho cha Taifa au mpigakura au leseni ya udereva.

Mtumishi huyo pia atatakiwa kujaza hati ya ridhaa kwa aliyekuwa mwajiri wake.

## Wauguzi matatani kwa tuhuma kugoma kumhudumia mjamzito

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKAZI wa Mlombo mjini Babati, Sophia Bakari amedai kujifungua wodini kwa kusaidiwa na dada yake baada ya wauguzi waliokuwa zamu kwenye Hospitali ya Wilaya ya Babati kugoma kumhudumia wakidai anapaswa kusubiri mpaka wamalize kula.

Kutokana na tuhuma hizo, uongozi wa hospitali hiyo umeanza kufanya uchunguzi ili kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa wauguzi hao watabainika kutenda kosa hilo.

Sophia (36) anadai alifika hospitalini huko Desemba 17 mwaka huu majira ya saa tano usiku akiwa ameshikwa na uchungu wa kujifungua na aliwakuta wauguzi wawili ambao badala ya kumhudumia, walimwambia wanakula, hivyo atangulie wodini akajichagulie kitanda.

Katika mazungumzo na Nipashe mjini hapa juzi, mzazi huyo aliiomba Wizara ya Afya na uongozi wa Mkoa wa Manyara kufuatilia tukio hilo ili kuongeza uwajibikaji kwa watumishi wa kada ya afya.

"Baada ya kufika hospitalini, niliambiwa niingie wodi ya wazazi nikachague kitanda nilale. Nilitii kwa kufanya hivyo na uchungu ulipozidi, niliwaita wauguzi wanisaidie, ila walikaidi kwa kugoma kunihudumia.

"Nilipowauliza mbona hawaji kunihudumia, waliniambia kama nina haraka niende Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara. Nilikataa nikasema 'uchungu umechanganya', nikaingia chumba cha kujifungulia na akanifuata dada yangu ambaye alinisaidia kunizalisha," alisimulia Sophia.

Mzazi huyo alidai alishangaa kuambiwa na wauguzi hao aende kujifungua kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara pasi na kukagua kadi yake ya kliniki wala kusoma historia ya maendeleo ya ukuaji wa mtoto.

Mama huyo aliyejifungua mtoto wa kike, alidai kuwa baada ya kujifungua, aliulizwa na na wauguzi hao kama alihitaji wamuuzie soksi kwa ajili ya mtoto na mrejesho wake kwao ni kwamba alikuwa anazo.

Mume wa Sophia, Hamis Katuga (65) alidai mke wake alikataliwa toka mwanzo na hospitali hiyo kupatiwa huduma ya kliniki, hivyo kulazimika kuipata kwenye zahanati ya kanisa.

Alidai kuwa alishangazwa na wauguzi wa zamu kwenye hospitali hiyo ya wilaya kutaka kumpa rufani mke wake kwenda kupata matibabu Hospitali ya Rufani ya Mkoa bila hapa kumpima.

**KAULI YA HOSPITALI**

Alipotafutwa na Nipashe kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko hayo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Halima Mangiri alikiri kuwapo malalamiko ya mgonjwa huyo.

Hata hivyo, Dk. Mangiri aliahidi kutoa taarifa wakati wowote baada ya uchunguzi wa tuhuma hizo kukamilika.

"Ni kweli ofisi yangu imepokea malalamiko ya mwanamke huyo na tumeanza kufanya uchunguzi na tutakapobaini wahusika wa zamu siku hiyo walifanya makosa hayo, watachukuliwa hatua za kinidhamu," aliahidi.

## HABARI KITAIFA

# Mtoto wa miaka 6 adaiwa kujinyonga

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MTOTO aliyetambulika kwa jina ya Tumaini Emmanuel (6) anadaiwa kufariki dunia baada ya kujinyonga kwenye mti wa mwembe wakati akibembea.

Tukio hilo limetokea jana kijijini Ndurumo, barabara ya nne kwenye Halmashauri ya Nsimbo mkoani Katavi.

Inadaiwa kuwa mtoto huyo alikuwa nyumbani kwao na ni kawaida yake kucheza kwenye mti huo akifunga kamba juu ya mti na kuanza kubembea.

Wakati tukio hilo likitokea, wazazi wake walikuwa shambani na hakuna mtu yeyote aliyekuwa karibu na nyumba yao zaidi hadi pale wapita njia walipoona mwili wake ukiwa juu ya mti.

Wakizungumzia kifo cha mtoto wao, wazazi walisema taarifa hizo wamezipata wakiwa shambani kwa kuwa nyumbani alibaki mtoto aliyepoteza maisha pamoja na dada yake.

"Mimi sikuwapo nyumbani, mtoto alikwenda kujining'iniza kwenye kamba hapo juu ya mwembe, alikuwa anabembea, nimesikia alikuwa amejifunga kamba shingoni," alisema baba wa mtoto huyo, Emmanuel Kagoma.

"Binti yangu alikuwa na miaka sita. Mimi nilikuwa shambani, yeye alibaki nyumbani na dada yake, baadaye watu walipomwona walimwita dada yake aje amwone mdogo wake alivyojining'iniza kwenye kamba.

"Hapakuwa na ugomvi wowote, alikuwa akicheza alifunga kamba moja juu ya mti, sasa wakati akibembea aliingiza shingo kwenye kamba huku miguu ikiwa chini basi ndiyo hayo yakatokea," alieleza mama wa mtoto, Juliana Kiana.

Baadhi ya majirani walisema matukio kama hayo wamezoea kuyasikia kwa watu wazima na siyo kwa watoto kama ilivyotokea katika familia hiyo, hivyo wameshangazwa na tukio hilo.

"Tukio hili tumelipokea kwa mshangao kwa kweli, sababu mtoto alikuwa mdogo ambaye hawezi kufikia uamuzi kama huo, yaani ni jambo ambalo haliingii akilini tunawaza nini kimemsibu mtoto hadi ikawa hivyo.

"Lakini katika hali ya kuulizia katika huo mti tumeambiwa alikuwa akipenda sana kuchezea hapo akitumia kamba kama bembea, tunachohisi kwa kuwa alikuwa peke yake aliona hana mtu wa kumsukuma katika bembea hiyo akahisi kwamba atakapoweka ile kamba shingoni atabembea kwa urahisi.

"Kulingana na mazingira waliokuwa wakiishi watoto na familia yake na majirani hatujafikiria sana kama kunaweza kuwa na ushirikina umetokea, wito wangu kwa wazazi watoto wanahitaji sana uangalizi wa karibu hata katika michezo wanayocheza," alisema Lucas Jakobo.

Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Ndurumo, Martine Salungi alisema alipokea taarifa za tukio hilo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kitongoji majira ya saa tano asubuhi akiwa shambani, akitakiwa awahi eneo la tukio.

"Baada ya kufika, nilikuta mtoto ameshajinyonga akiwa kwenye mti amefunga kamba ya chandarua, basi tulifanya uamuzi mimi na viongozi wenzangu tulipiga simu kituo cha polisi.

"Polisi walifika pamoja na mganga wakafanya uchunguzi wao kama wataalamu, walipomaliza walituruhusu sisi kama familia tuzike na wao wakaondoka," alisema Martine Sarungi.

Mwili wa mtoto Tumaini Emmanuel ambaye alikuwa akisoma darasa la awali, ulizikwa nyumbani kwao ikiwa ni hatua chache kutoka usawa wa nyumba yao wanayoishi huko kwenye Kijiji cha Ndurumo.

# Kizimbani kwa mashtaka biashara dawa za kulevya

**Na Grace Gurisha**

WAKAZI watatu wa jijini Dar es Salaam, akiwamo mwanamke, wamefikishwa kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kukutwa wakifanya biashara ya dawa za kulevya aina ya heroine kilogramu 15.19.

Wakazi hao ni Suleman Thabiti, Sharifa Bakari na Faridi Said, wote wakazi wa Dar es Salaam ambao walifishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa mahakama hiyo kwa ajili ya kusomewa mashtaka yao.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Tumaini Mafuru alidai mbele ya Hakimu Mrio kuwa washtakiwa wanatuhumiwa kwa kosa la kufanya biashara ya dawa za kulevya kinyume cha sheria.

Alidai kuwa Novemba 29 mwaka huu, washtakiwa, wakiwa eneo la Mbagala Chalambe, mkoani Dar es Salaam, walikutwa wakifanya biashara ya dawa za kulevya aina ya heroine kilogramu 15.19.

Baada ya washtakiwa kusomewa shtaka hilo, hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo. Mahakama Kuu ndiyo yenye mamlaka hayo.

Mafuru alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Kesi hiyo itatajwa Januari 6 mwakani na washtakiwa walirudishwa rumande kwa sababu kisheria mashtaka ya aina hiyo hayana dhamana.


MKOMBOZI COMMERCIAL BANK
a bank with integrity

**MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC**

**New Rates-VAT Exclusive**
**Effective dates .......... Toll-free: 0800 750 040**

| | Product | Previous Charge | New Charge |
|---|---|---|---|
| Minumum account opening balance | Personal Current Account | 15,000 | 50,000 |
| | Intergrity Account | 20,000 | 50,000 |
| Minumum account operating balance | Intergrity Account | 10,000 | 50,000 |
| | Forex Account $/£/€ | 50 | 100 |
| Interest payable - below 5Mln balance on savings account<br>Interest payable - above 5Mln balance on savings account | Business Savings Account | n/a | n/a |
| Monthly maintainance fees | Business Current Account | 12,000 | 18,000 |
| | Personal Current Account | 10,000 | 12,000 |
| | Business Savings Account | 1,500 | 5,000 |
| | Personal Savings Account | 1,500 | 5,000 |
| | Joint Account | 2,000 | 3,000 |
| | Wajasiriamali Account | Free | 3,000 |
| | Forex Account $/£/€ | Free | $/£/€ 10 |
| | Salary Account | Free | 1,500 |
| Teller withdraw fee below TZS 5Mln | Business Current Account | 4,000 | 6,000 |
| | Personal Current Account | 4,000 | 5,000 |
| | Call Account | Free | 5,000 |
| | Business Savings Account | 4,000 | 5,000 |
| | Student Account | 1,500 | Free |
| | Joint Account | 4,000 | 5,000 |
| | Mwana Account | 4,000 | 3,000 |
| | Wajasiriamali Account | Free | 3,000 |
| | Salary Account | Free | 3,000 |
| Teller withdraw fee above 5Mln - 20Mln | Business Current Account | 6,000 | 8,000 |
| | Personal Current Account | 6,000 | 7,000 |
| | Call Account | Free | 7,000 |
| | Business Savings Account | 6,000 | 7,000 |
| | Student Account | 5,000 | Free |
| | Joint Account | 6,000 | 7,000 |
| | Mwana Account | 6,000 | 5,000 |
| | Wajasiriamali Account | Free | 5,000 |
| | Salary Account | Free | 5,000 |
| Teller withdraw fee above 20Mln | Call Account | Free | 0.12% min - 100,000 Max |
| | Student Account | 0.12% min - 100,000 Max | Free |
| | Salary Account | Free | 0.12% min - 100,000 Max |
| Teller B/E | Student Account | 500 | Free |
| Certificate of Balance | Student Account | 30,000 | Free |
| Confirmation to Auditors | Student Account | 30,000 | Free |
| Cheque book costs per leaf | All current accounts | 500 | 1,000 |
| | Community Current Accounts | Free | 1,000 |
| Dishonoured Cheque due to technical error | Community Current Accounts | 30,000 | Free |
| | Personal Current Account | 30,000 | Free |
| Dishonoured Cheque due to insufficient funds | Community Current Accounts | 150,000 | 75,000 |
| | Personal Current Account | 150,000 | 75,000 |
| Monthly charges drawn below minimum balance | Student Account | 10,000 | Free |
| Salary processing/bulk payment (per entry) | Business Current Account | Free | 500 |
| | Business Savings Account | Free | 500 |
| SMS Alert | All accounts with SMS alert service | 100 | 150 |
| Standing order instruction within MKCB | Community Current Accounts | 5,000 | Free |
| | Student Account | 5,000 | Free |
| Standing order instruction to other Bank | Student Account | 15,000 | 5,000 |
| Unpaid Bankers' Order | Student Account | 30,000 | Free |
| ATM Card | New | 5,000 | 15,000 |
| | Replacement | 10,000 | 15,000 |
| ATM Withdraw fee | Umoja Switch | 1,300 | Up to 49,999 – 1,400<br>Above 49,999 - 400,000 – 1,700 |

**Note: These charges are exclusive of Government Levy**

17205801

HABARI KITAIFA

# Ataka bajeti kwa vituo vya malezi ya watoto

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

MKURUGENZI wa kituo cha kulea watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu cha Gain Upendo, Erick Ouma amesema kuna haja serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum kutenga bajeti kwa ajili ya kusaidia vituo vya kulea watoto.

Ouma ambaye anasimamia kituo hicho kilichoko Mlandizi, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, alitoa rai hiyo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu huduma zinazotolewa kwenye kituo hicho.

Alisema vipo vituo vimeanzishwa kwa lengo la kusaidia watoto hao lakini uwezo wa kuviendesha ni mdogo, hivyo kukiwa na utaratibu wa kusaidia, kutaondoa vikwazo vinavyojitokeza.

"Mfano, kwa sasa vitu mbalimbali pamoja na vyakula vimepanda bei tofauti na bajeti ya mwaka tuliyokuwa tumeiweka, hivyo kama serikali ingekuwa na utaratibu huo, itasaidia kuvisaidia pale inapotokea kikwazo," alifafanua.

Ouma alisema kwa sasa kituo hicho kina uhitaji wa magodoro 24 pamoja na vitanda, kikiwa na pia watoto 19 wanaosoma shule za msingi, sekondari na vyuoni pamoja na wasaidizi wao.

Alisema kituo hicho ambacho kilianzishwa mwaka 2014 kikiwa na watoto 18. Kati yao, wapo ambao tayari wamefika chuo kikuu wakisomeshwa na kituo hicho.

Kuhusu malezi ya watoto kwenye kituo hicho, mkurugenzi huyo alisema kumekuwa na utaratibu wa kuwakutanisha watoto kwenye kikao cha pamoja kuwaelimisha namna ya kuwajengea uwezo kukabiliana na vishawishi vinavyoweza kuwaweka kwenye hatari ya kupata mimba za utotoni.

# Mzee auawa kwa kukatwa panga imani za kishirikina zikitajwa

**Na Marco Maduhu**, SHINYANGA

MBALU Shija (68), mkazi wa Kijiji cha Mwalukwa wilayani Shinyanga, ameuawa kwa kukatwa panga kichwani akidaiwa mshirikina.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa saba usiku akiwa amelala nyumbani kwake kijijini huko.

Akisimulia tukio hilo jana, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwalukwa, Lucas Buchambi alisema tukio hilo lilitokea wakati wajukuu wake waliokuwa wakiishi nao walipokwenda kwa jirani kwa ajili kuimba kwaya kwa ajili ya mkesha wa Noel.

Alisema wajukuu wake waliporejea nyumbani usiku huo, mmoja ambaye hulala na bibi yake alipoingia chumbani akamwona bibi yao ameanguka chini akiwa ameuawa, ndipo akapiga kelele kuomba msaada.

"Baada ya kupata taarifa za tukio hili majira ya saa nane usiku, nilikwenda eneo la tukio na kumkuta bibi huyo akiwa ameuawa kikatili kwa kukatwa mapanga kichwani huku ubongo ukiwa nje.

"Chanzo cha tukio hili ni imani za kishirikina, marehemu alikuwa akituhumiwa kuwa ni mchawi na mhusika ambaye anatuhumiwa kutekeleza mauaji haya tayari ameshakamatwa na Jeshi la Polisi," alisema.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwalukwa, Elipendo John alilaani tukio hilo la kinyama na kueleza kuwa matukio ya mauaji ya kukata mapanga wazee yalikuwa yameisha mkoani Shinyanga, lakini anasikitika kuanza kuibuka upya.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi alithibitsha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa jeshi hilo linaendelea na uchunguzi wake.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania PLC, Philip Besiimire akisalimiana na Kamanda wa Trafiki nchini, SACP Ramdhani Ng'azi wakati kamanda huyo alipofika kujitambulisha katika Makao Makuu ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam na pia kufanya mazungumzo kuhusu namna bora ya kujenga uhusiano na vyombo vya usalama katika zama hizi za kidijitali, ziara hiyo imefanyika jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa asema serikali inaendelea kufanya maboresho makubwa MNH

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa amesema serikali inaendelea kufanya maboresho makubwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Majaliwa alisema hayo jana baada ya kufanya ziara katika hospitali hiyo na kuzungumza na wagonjwa na wauguzi ambao walimweleza kuwa huduma zinazotolewa hospitali hapo zinaridhisha.

Alisema katika kutimiza hilo, hivi karibuni imetoa fedha kwa ajili kununua vifaa vya kisasa ikiwamo mashine ya MRI ambayo inaweza kumpima mgonjwa hata akiwa na chuma mwilini.

"Sambamba na huduma hizi nzuri zinazotolewa na wataalam wetu kwa moyo mkubwa Serikali inaendelea kufanya maboresho makubwa katika hospitali yetu ya taifa ili iendelee kutoa huduma bora na za kisasa zaidi," alisema.

Waziri Mkuu pia alisema ameridhishwa na huduma za matibabu zinazotolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kuwapongeza watendaji wa hospitali hiyo kwa kuendelea kuwahudumia wagonjwa kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Kuhusu suala la gharama kubwa za matibabu ambalo limelalamikiwa na wananchi wengi wanaouguza ndugu zao, Waziri Mkuu alisema mpango wa bima ya afya kwa wote utakuwa suluhishi la changamoto hiyo.

Pia Waziri Mkuu aliwataka Watanzania ambao wanashindwa kumudu baadhi ya huduma za matibabu, wawasilishe masuala yao katika ofisi za ustawi wa jamii zilizoko kwenye hospitali husika na watapewa maelekezo ya kufuata ili wapate msamaha.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohammed Janabi, aliwasisitiza wagonjwa wote ambao hawana uwezo wa kulipia huduma mbalimbali zitolewazo hospitalini hapo, wafuate taratibu na watahudumiwa.

"Kila mwezi hospitali inatoa msamaha wa zaidi ya Sh. bilioni moja kwa wasiokuwa na uwezo," alisema Prof. Janabi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi wanaouguza ndugu zao katika hospitali hiyo wamesema kuwa huduma zitolewazo ni nzuri na hakuna anayeombwa rushwa ila changamoto waliyonayo ni kwamba matibabu yanatolewa kwa gharama kubwa.

Mmoja wa wanaoguza ndugu zao, Abia Mjule, alitumia fursa hiyo kuishukuru serikali kwa maboresho ya huduma ikiwamo misamaha ya matibabu inayotolewa kwa wagonjwa wasiokuwa na uwezo.

"Mjukuu wangu alilazwa Novemba 23, mwaka huu, na amefanyiwa upasuaji wa moyo ambao gharama yake ilikuwa Sh. milioni 4.26. Naishukuru serikali baada ya kuomba kupunguziwa, ilikubali na nikalipa nusu na nusu ililipwa na serikali," alisema.

# Mkoa wajipanga kuukabili utoro shuleni mwaka 2023

**Na Mwandishi Wetu**

MKOA wa Dodoma umejidhatiti kukabiliana na utoro wa wanafunzi shuleni kupitia maazimio yaliyowekwa kwa mwaka 2023 kupitia kikao cha pili cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kilichofanyika juzi chini ya Mwenyekiti wake, Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma.

Katika kikao hicho, agenda ya elimu ilijadiliwa kwa kina na kupewa msukumo madhubuti ikiwa ni miongoni mwa ajenda nane za kikao hicho kilichojadili masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwamo bajeti ya mkoa na sekta za elimu, afya, kilimo, maji na mazingira.

Ilibainishwa wakati wa kikao hicho kuwa Mkoa wa Dodoma unakabiliwa na changamoto kubwa ya utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari huku sababu kubwa zikitajwa kuwa ni ukosefu wa chakula shuleni, wazazi/walezi kutoipa thamani stahiki elimu hivyo kutowajibika kwa malezi ya watoto wao, viongozi wa vijiji kushindwa kutimiza wajibu wao wa kudhibiti utoro shuleni na umbali mrefu wa kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary, alisema licha ya changamoto hizo katika sekta ya elimu, Wilaya ya Bahi imefanya vizuri kitaifa katika matokeo ya darasa la saba mwaka huu.

"Ninaipongeza sana Halmashauri ya Bahi kwa kushika nafasi ya juu kwa mpangilio wa ufaulu wa halmashauri kitaifa kwani wameupa fahari Mkoa mzima wa Dodoma. Ninatoa shime kwa halmashauri nyingine kwenda kujifunza Bahi namna walivyofanya na kufanikiwa kuingia kwenye 10 bora za kitaifa. Pia tukafanye kazi kubwa kuhakikisha watoro wanarudi shuleni mwaka 2023," aliagiza.

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga alitoa rai kwa wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kutoa msukumo kwa walimu kufundisha kwa bidii kwa lengo la kuongeza kiwango cha ufaulu.

Akitoa maoni yake kuhusu maazimio ya mwaka 2023, Ofisa Elimu Mkoa, Gift Kyando alisema: "Mwaka ujao tunaazimia wanafunzi wote watakaomaliza elimu ya msingi kurudi mapema shuleni kwa ajili ya kujiandaa na masomo ya kidato cha kwanza tofauti na ilivyokua mwaka huu kwani mitihani ilichelewa badala ya kufanyika mwezi Septemba imefanyika mwezi Oktoba ila mwakani itafanyika kama kawaida mwezi Septemba."

Katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary, aliziagiza halmashauri kuongeze kasi ya kukusanya mapato na kutoa asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya mikopo ya makundi maalum.

"Ninaziagiza halmashauri zote kwa kushirikiana na wadau kuendelee kutengeneza madawati ili kupunguza upungufu uliopo, halmashauri zikamilishe usimamizi wa sheria ndogo za upatikanaji wa chakula shuleni pamoja na kudhibiti utoro, kila shule itenge eneo la kuzalisha chakula kwa wanafunzi, vyuo vya ufundi viimarishwe," aliagiza.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na wagonjwa wakati alipotembelea Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU,**

# DC awaonya wazazi kutumikisha watoto

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Sophia Kizigo amewaonya wazazi dhidi ya tabia ya kutumikisha watoto kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kuchunga ng'ombe.

Alitoa onyo hilo juzi wakati wa hafla ya kukabidhi madarasa 18 wilayani humo kwenye Shule ya Sekondari Iguguno iliyoko Kata ya Iguguno.

Alisema kuwatumikisha watoto kazi za kuchunga mifugo na kusababisha wasiende shuleni ni kurudisha nyuma juhudi za serikali ambazo zinalenga kutoa elimu bora kwa watoto.

"Ninaomba mtafute watu wengine wa kuchunga, siyo watoto wenu, waacheni waende shuleni, la sivyo madarasa haya mengi niliyopokea yatakosa maana kama watoto wenu hawataenda shuleni," aliagiza.

Kizigo alisema wazazi wanatakiwa kuwekeza kwenye elimu ili kuwa na taifa la wasomi watakaoshika nyadhifa mbalimbali nchini.

Vilevile, aliwataka wazazi wote wilayani humo kuunga mkono juhudi za serikali ambayo imekuwa ikitoa fedha nyingi kutekeleza miradi ya elimu kwa kuhakikisha ifikapo mwezi Januari mwakani kila mtoto aliyechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza anaripoti shuleni mapema.

"Serikali inatujali sana wananchi wa Wilaya ya Mkalama, leo (juzi) nimepokea madarasa 18 na ofisi moja ya walimu, hakika mama (Rais Samia) ameupiga mwingi!

"Ninaomba tuhakikishe tunawekeza kwenye elimu, unajisikiaje Mkuu wa Wilaya akatoka Mkalama? Mtajisikiaje watoto wenu wa Mkalama wakawa mahakimu wa wataalamu wa kilimo watakaolima kwa tija kwa maslahi ya Wilaya?" Mkuu wa Wilaya alihoji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos alisema halmasahauri yake ilipokea Sh. milioni 340 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 17 vya madarasa ya wanafunzi wa kidato cha kwanza waliochaguliwa kujiunga na sekondari kwa mwaka 2023 ambayo yote ujenzi wake umekamilika.

Alisema kutokana na ushiriki wa wananchi kujitoa nguvu kazi, fedha zilizotolewa zimechonga viti na meza seti 375, kuongeza chumba kimoja cha darasa kwenye Shule ya Sekondari Iguguno pamoja na ofisi moja ya walimu, hivyo kufanya jumla ya madarasa 18 na ofisi ya walimu.

Baadhi ya wananchi walioshiriki hafla hiyo, waliipongeza serikali kwa kujenga madarasa hayo, wakiamini yatainua kiwango cha elimu wilayani Mkalama huku wakiiomba serikali kuongeza walimu ili kuweka uwiano sawa kati ya wanafunzi na walimu.

Shule zilizojengewa madarasa mapya ni Sekondari za Chemchem iliyoko Kata ya Mpambala, Malaja iliyoko Kata ya Nkalakala, Seth Benjamini iliyoko Kata ya Nkalakala, Selenge ya Kata ya Mwanga, Gracemesaki ya Kata ya Kinampundu, Kikhonda ya Kata ya Kikhonda, Kinto ya Kata ya Nkinto, Iguguno ya Kata ya Iguguno, Kinyangiri ya Kata ya Kinyangiri na Ibaga ya Kata ya Ibaga.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 2444/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HALFANI JUMA SENYANGE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HAWA HALFANI SENYANGE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 Mwezi wa 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 23 Mwezi wa 12 Mwaka 2022.**

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya MOROGORO**
**Kituo cha Chamwino Mkoa wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 30/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU SALEHE SEKISASA KAMNGE WA MOROGORO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA HAWA PONSIANO IBRAHIM**

**TANGAZO**
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **04**/ Mwezi **01** Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 23 mwezi 12 mwaka 2022**

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT LTD**
**NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT** kwa idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama zilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku saba (7) kuanzia tarehe ya Notisi/ Tangazo hili endapo hatalipa deni lake.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | GAIMO CONSTRUCTION COMPANY LIMITED | GAUDENCE VICENT LYIMO AND MONICA GAUDENCE LYIMO | NYUMBA YENYE HATI YA MAKAZI Na. 21393, PLOT No. 407, BLOCK 'JJ' OLOIRIEN, MANISPAA YA ARUSHA, ARUSHA | 31.12.2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/ dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/ eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**
**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT**
**P.o.Box 11898, ARUSHA**
**Tel: 0784 200283/ 0744 205017**
**Email: harvestercapital558@gmail.com**

**IN THE DISTRICT COURT OF NACHINGWEA**
**AT NACHINGWEA**
**MOTRIMONILA CAUSE NO. 05 OF 2022**
**BETWEEN**
**DAINES SANDI MAKOTHA............PETITIONER**
**VERSUS**
**MADUHU SAMSON MAONGO.........RESPONDENT**

**TO: MADUHU SAMSON MAONGO**
**P.O.BOX 291**
**NACHINGWEA.**

**WHERE** the above **MATRIMONILA CAUSE** is set down for judgement on **23rd** day of **December, 2022** at **09:00 o'clock** in the morning soon.
Thereafter, you are hereby summoned to appear before this court without fail.
In case you default to enter appearance the petition may be heard ex- Parte or dismissed.
A copy of application attached herewith.
Given under my hand and the seal of the court this **21st** day of **December, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE
NACHINGWEA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba,**
**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa wa Kagera**
**Shauri la Madai Na. 20/2022**
**Jina la Mdai ...........Julius Kashangaki**
**Jina la Mdaiwa ........Adinani Haruna**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**

**KWA ADINANI HARUNA,** Kwamba Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe **05 Mwezi 01 Mwaka 2023** kueleza kwa nini hukumu isitekelezwe dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe **22 Mwezi 12 Mwaka 2022.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA BUKOBA
BUKOBA MJINI

**Company No. 133552**
**RIVAAS DISTRIBUTORS LIMITED,**
**P.O. Box 10539**
**ARUSHA - TANZANIA**

EXTRACT OF THE RESOLUTION OF AN EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING OF THE MEMBERS OF RIVAAS DISTRIBUTORS LIMITED HELD AT THE COMPANY REGISTERED OFFICE ON THE 10TH DAY OF JULY, 2021.
THE FOLLOWING RESOLUTION WAS DULY PASSED RESOLUTION
It was RESOLVED by the members of the Company that the Company Be wound Voluntarily.
**Dated at Arusha this 10TH day of JULY, 2021.**

CHAIRPERSON
COMPANY SECRETARY

RIVAAS DISTRIBUTORS LTD.
P. O. BOX 10539
ARUSHA

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu kuweni makini dirisha hili la usajili

**DIRISHA** dogo la usajili lipo wazi kwa sasa na klabu zipo kwenye pilika za kutaka kuboresha vikosi vyao.

Kila ukimsikia kocha wa timu analalamika udhaifu kwenye baadhi ya maeneo ya kikosi chake. Ni klabu moja tu ambayo nimemsikia kocha wake akisema kuwa hahitaji kufanya usajili kwa sababu ana kikosi kipana. Huyo ni Kocha Mkuu wa Azam, Kalimangonga Ongala.

Lakini klabu zote zilizobaki zimeonekana kuwa na mapungufu na zikilalamika kuwa ikifika kipindi cha usajili wa dirisha dogo ni lazima waongeze nguvu kwenye vikosi vyao.

Kuanzia Simba, Yanga, Ihefu hadi Dodoma Jiji, nina maana timu 15 zilizobaki zinaonekana kuwa na uhitaji wa kuongeza nguvu vikosi vyao.

Yanga ambayo nayo ina straika wake hatari kabisa nchini, Fiston Mayele inaonekana nayo itasaka mshambuliaji kwa sababu haina mbadala wake kama akiumia au kupatwa na tatizo lolote litakalomuweka nje. Timu nyingi zina washambuliaji, lakini hazina wafungaji kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Ihefu, Juma Mwambusi, akiongeza kuwa watu wa aina hiyo adimu sana.

Mwinyi Zahera naye akasema kuwa anahitaji straika mwenye uwezo wa kufunga mabao manane hadi 10 kwa msimu na si mradi straika tu.

Hii inaonyesha kuwa dirisha hili dogo linaweza kuwa na vita kali kama lilivyo dirisha kubwa. Kunyang'anyana wachezaji na michezo mingine isiyo ya manufaa kwenye mchezo wa soka inaweza kufanyika kwa sababu inaonekana kuwa dirisha ni dogo na mahitaji ni makubwa.

Ndiyo maana Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kupitia Afisa Habari na Mawasiliano, Cliford Ndimbo akatoa rai kwa klabu na wachezaji jinsi ya kulitumia dirisha hilo, pamoja na kutoa onyo.

Dirisha dogo ni wakati wa kuongeza nguvu au kuimarisha kikosi, siyo wa kusajili kikosi kizima, tumeshatoa semina ni jinsi gani usajili huu unatakiwa kufanyika mwanzoni mwa msimu mameneja waliitwa, naamini kwa kipindi hiki chote hakutakuwa na changamoto yoyote katika eneo hilo la kusajili," akasema Afisa Habari na Mawasiliano huyo na kuongeza.

"Tunatoa nafasi kwa klabu yoyote ikipata changamoto wakati ya kusajili au kuhamisha mchezaji, basi wawasiliane na TFF ili kuhakikisha changamoto zao zinatatuliwa kabla ya dirisha kufungwa. Dirisha ni mwezi mmoja, klabu zitumie muda vizuri, waache ule mtindo wao wa kusubiri hadi siku za mwisho ndiyo wanaanza kuhangaika kufanya usajili, muda unaruhusu na zile klabu ambazo zitasajili wachezaji ambao bado wana mikataba na wachezaji watakaosaini mara mbili, bahati nzuri kanuni zipo wazi na zitahusika kuwahukumu," alisema.

Tunatarajia klabu zitasajili wachezaji ambao wanawahitaji, lakini pia kwa kufuata taratibu ili kuepuka mambo ya kusajili wachezaji ambao wana mikataba na klabu zingine kama ilivyojitokea kwenye dirisha kubwa pale Singida Big Stars ilipomsajili kipa Metacha Mnata akiwa na mkataba na Polisi Tanzania na Prisons ikamsajili kipa Musa Mbisa aliyekuwa bado ana mkataba na Coastal Union.


Kilichotokea ni kwamba wachezaji hao waliruhusiwa kuchezea klabu zao mpya, lakini zikifungiwa kusajili dirisha hili dogo, ingawa tayari adhabu hizo zimeondolewa kwa kupewa adhabu zingine mbadala.

Wachezaji nao wanatakiwa kuwa makini, wasiingize klabu mkenge. Kama wana mikataba na klabu zao, waseme ili zile zinazowataka zifuate utaratibu na si kusema uongo.

Kwa upande wa TFF na Kamati yake ya Sheria na Hadhi za wachezaji inatakiwa itende haki kwa pande zote na si kuzionea klabu ndogo. Mchezaji wa klabu ndogo anaweza kuchuliwa na klabu kubwa bila utaratibu lakini ukakuta iliyochukuliwa haitendewi haki kwa sababu ya maslahi wa klabu kubwa, huu ni uonevu.

Kama klabu zitatuliza kichwa na kuwa makini kwa kila kitu, nadhani linaweza kupita salama bila malalamiko yoyote na tunaombea iwe hivyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Marefa Ligi Kuu wawe wakali kwa wachezaji wenye rafu

**MMOJA** wa mabosi wa waamuzi wa Kombe la Dunia lililoisha hivi majuzi nchini Qatar, Pierluigi Collina kabla ya michuano hiyo alitoa semina kwao ambayo ilikuwa ikiwataka kuwalinda wachezaji wanaotaka kucheza soka.

Collina ni mwamuzi wa zamani Muitaliano ambaye anakumbukwa kwa kuwa mmoja wa marefa wakali, wenye maamuzi magumu, aliyeogopwa na wachezaji wote wakiwemo mastaa wa dunia hii kutokana na uchezeshaji wake murua, na maamuzi ya haki na halali.

Huyu jamaa anakumbukwa sana na mashabiki wengi wa soka wa Tanzania kwa sababu miaka ambayo televisheni mwishoni mwa miaka ya 1990 ndiyo zimeanza kuingia na kuonyesha mipira alikuwa ndiyo refa mahiri akichezesha mechi tata, kubwa na zenye mvuto.

Alikaa na waamuzi kabla ya Kombe la Dunia na kuwaambia wawalinde sana wachezaji ambao wanataka kucheza soka na kutoa burudani kwa watu wote waliokata tiketi ya kuangalia michuano hiyo. Mpira ni burudani, siyo ugomvi wala uhasama. Waamuzi wawe wakali na wasisite kuwachukulia hatua wachezaji ambao kwa makusudi wanaacha kucheza soka na kuhatarisha maisha ya wanasoka wenzao.

Akaenda mbali akisema, mwamuzi yeyote asisite kumtoa nje kwa kadi nyekundu mchezaji ambaye anaonekana hata tu kwamba ana dhamira mbaya dhidi ya mchezaji mwenzake.

Hii ikanikumbusha mwamuzi mmoja wa zamani aliyemtoa nje mchezaji kwa kadi nyekundu bila hata buti lenyewe kumpata mchezaji aliyechezewa.

Mchezaji alipomfuata na kumwambia kwa nini amempa kadi nyekundu wakati hata kwanja halijampata alijibu neno moja tu lililojibu kila kitu, 'dhamira'.

Ina maana dhamira ya mchezaji huyo haikuwa nzuri, ilikuwa ni kumuumiza mchezaji wenzake, hivyo mwamuzi alichofanya ni kumlinda ili baadaye asije akaumizwa.

Kwenye Ligi Kuu ya Tanzania kwa sasa waamuzi wanaonekana wao kazi yao ni kuchezesha mechi tu na si nyingine.

Waamuzi hawalindi afya za wachezaji kwa kuachia rafu za ovyo, ambazo nina uhakika waamuzi wa zamani kama kina Othman Kazi, Israel Nkongo, Abdulrasul Ismail, Omar Abdulkadir wasingeweza kuzifumbia macho.

Sijajua waamuzi wa sasa wanakumbwa na matatizo gani, lakini jambo la kwanza wanaanza kuwa na wasiwasi na mechi, au presha wanapochezesha kuliko wachezaji wenyewe wanaocheza.

Hawana mamlaka uwanjani, ndiyo maana wanaweza kubishana na wachezaji na kusukumwa bila kutoa kadi.

Nimeona hivi karibuni mchezaji Charles Ilamfya akimchezea mmoja wa wachezaji wa Namungo rafu mbaya. Hii kadi nyekundu ilitoka, lakini Shiza Kichuya alitoa rai kwa wachezaji kulindana wenyewe kwa wenyewe kabla waamuzi hawajawalinda.

Ni kweli kabisa, lakini kuna baadhi ya wachezaji wakishashindwa uwezo wa kumdhibiti mchezaji wa timu pinzani basi anachofanya ni kumchezea rafu, ambayo pia inahatarisha maisha yake ya soka.

Mpira ni kazi kama nyingine yoyote na wachezaji wanategemewa na familia zao ili waishi kwa kazi hiyo, hivyo waamuzi wanatakiwa walijue hilo.

Mashabiki wanakwenda uwanjani na wanajazana kuangalia vipaji na uwezo wa wachezaji, hivyo anapotokea mwingine anazuia kwa maguvu na fujo, huo sasa siyo mpira.

Tumeona hata wachezaji kina Fiston Mayele wa Yanga na Mosses Phiri wa Simba wakichezewa rafu mbaya, lakini hakuna juhudi zozote za kuwalinda. Na siyo hao tu, hata wengine pia wanatakiwa kulindwa.

Wachezaji wanapoona mwamuzi hawalindi, hawawezi kuwa huru kutoa burudani kwa mashabiki, matokeo yake soka linakuwa halina ladha.

Zamani waamuzi walikuwa kwanza wanajua mechi ya leo anakwenda kuwachezesha wachezaji wa aina gani, timu fulani na fulani ina mastaa gani na ina wachezaji wakorofi kina nani.

Hapo waamuzi wanakuwa makini sana kuwalinda wachezaji wastaarabu dhidi ya wakorofi ambao wanacheza rafu nyingi.

Mwamuzi mmoja aliwahi kuniambia ili uwe bora ni lazima ujue tabia za wachezaji unaokwenda kuwachezesha, wachezaji ambao wao wanachojua ni soka tu, walalamishi, wacheza rafu, wakorofi, na hata wanaopenda kujiangusha, hii inamfanya kuanza kuwadhibiti mapema anapoona tabia zao zimeanza kujitokeza na hasiti kuchukua hatua mapema kabla hawajamharibia mechi.

***Waamuzi wa kisasa wanakwama wapi? Kwa nini hawawalindi wachezaji? Wanataka hadi wavunjike miguu au wafie viwanjani?***

# Malori yakamatwa tuhuma za kusafirisha kemikali magendo

**Na Samson Chache,** TARIME

MAOFISA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Mara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, wayanashikilia malori mawili kwa madai ya kusafirisha kemikali kinyume cha sheria.

Magari yaliyokamatwa na ambayo yako chini ya mamlaka hizo ni gari la mafuta (tanker) lenye namba za usajili T191 CTB na tela lake namba T 823 DHC na lori aina ya TATA lenye namba T 967 DNX.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mara, Adam Ntoga, alisema: "TRA Mkoa wa Mara kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Kupambana na Biashara za Magendo na Uhujumu Uchumi usiku wa kuamkia Desemba 23, 2022, tukiwa katika doria barabara kuu ya Mwanza hadi Sirari katika Daraja la Mto Mara, Kirumi, tulikamata gari aina ya TATA lenye namba T 967 DNX likiwa na mapipa ya kemikali spiriti lita 1,200.

"Na usiku huo pia katika barabara hiyo Kituo cha Komaswa, tulilikamata lori la mafuta lenye namba za usajili T 191 CTB na tela lake lenye namba T 823 DHC la Kampuni ya Lukase Ltd likiwa na kemikali spirit lita 41,000 yakisafirisha kwenda Sirari bila kufuata utaratibu na kuwa na kigugumizi inakopelekwa spiriti hiyo kuuzwa," alisema Adam Ntonga, Meneja wa TRA Mkoa wa Mara.

Alisema baada ya kuwakamata, waliweahoji madereva hao wanakopeleka kemikali hiyo, leseni ya biashara, kodi na ushuru mbalimbali na kama wamelipia ushuru na wanunuzi kwa kuwa kumekuwapo na wafanyabiashara mbalimbali wanaokwepa kulipa kodi.

"Yeyote yule anayejua anahusika kwenye kemikali hiyo tunamwomba afike TRA kutoa maelezo. Tumejaribu kuwapigia simu watu wanaotajwa lakini simu zao hazipatikani. Tunwaomba wajitokeze kutoa maelezo ya ufafanuzi kwak uwa lori aina ya TATA lilivyo haliruhusiwi kubeba kemikalim," alisema.

Kamanda wa Polisi Tarime Rorya, Kamishna Msaidizi (ACP) Geoffrey Sarakikya alikiri kukamatwa kwa magari hayo na kwamba yako chini ya TRA Kituo cha Sirari na uchunguzi unaendele.

**Magari yaliyokamatwa na ambayo yako chini ya mamlaka hizo ni gari la mafuta (tanker) lenye namba za usajili T191 CTB na tela lake namba T 823 DHC na lori aina ya TATA lenye namba T 967 DNX.**

# Bilioni 5/- zatolewa kuiboresha miundombinu ya elimu Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeupatia Mkoa wa Dodoma Sh. bilioni tano kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule za msingi na sekondari.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dodoma, Mwalimu Gift Kyando alibainisha hayo juzi alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa sekta ya elimu katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

"Oktoba 31 mwaka huu mkoa kupitia halmashaurin zake ulipokea Sh. bilioni tano kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari, ni jukumu la kila halmashauri na kila mdau kusimamia na kufuatilia matumizi sahihi ya fedha hizo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa," aliagiza.

Kyando pia alisema Mkoa wa Dodoma unakabiliwa na kero kubwa ya utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Alitaja sababu za utoro kuwa ni pamoja na ukosefu wa chakula shuleni, wazazi/walezi kutoipa thamani inayostahili elimu, viongozi wa vijijini kushindwa kutimiza wajibu wao wa kudhibiti utoro shuleni na umbali mrefu kwenda na kurudi shule.

"Hadi kufikia Oktoba 28 mwaka huu jumla ya wanafunzi 18,083 (13,083 ni wa shule za msingi na 5,602 wa sekondari) sawa na asilimia 2.5 walibainika kuwa ni watoro wa zaidi ya siku 90," alibainisha.

Ofisa Elimu huyo alisema mkoa ulipokea Sh. bilioni 6.7 kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 339 kwenye shule za sekondari.

Alisema fedha hizo zimetolewa ili kufanya maandalizi ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza wa mwaka wa masomo 2023.

"Ujenzi wa madarasa hayo 339 kwenye halmashauri zote umekuwa katika kasi nzuri inayoashiria kazi hiyo kukamilika kwa wakati," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Dodoma waliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuinua kiwango cha elimu katika mkoa huo.

Mkazi wa Kata ya Chang'ombe, Furaha Danson alisema kuwa baada ya serikali kuwekeza katika kuboresha miundombinu ya elimu, matunda yamenza kuonekana katika matokeo ya mwaka huu ambapo Wilaya ya Bahi imeingia katika orodha ya halmashauri 10 bora kitaifa.

Alisema serikali imeendelea kutoa fedha, hivyo katika kipindi cha miaka mitatu ijayo ana matumaini nchi itakuwa umepiga hatua kubwa kwenye sekta ya elimu.

Mfanyabiashara wa Matunda Soko la Majengo, Fatuma Issa alisema serikali imepunguza mzigo kwa wazazi kwa kuwa hivi sasa kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita hakuna ada, lakini kuna haja kuchukua hatua dhidi ya 'utiriri' wa michango shuleni.

Alisema kazi imebaki kwa wanafunzi kuzingatia mambo ya shuleni ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao.



Diwani wa Viti Maalum Ilala Dar es Salaam, Beatrice Edward, akichangia hoja katika mkutano wa kujadili mikakati ya kukabiliana na vitendo vya ukeketaji kwenye Kata ya Mzinga na maeneo mengine wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCAA-CCC yawaahidi huduma bora wadau wa usafiri wa anga

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA-CCC) limesema litaendelea kuhakikisha watumiaji wa huduma za usafiri wa anga nchini wanapata huduma kwa wakati na kufurahia safari zao.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Innocent Kyara katika salamu zake za Mwaka Mpya wa 2023.

"Kama kaulimbiu yetu inavyosema 'Haki Zako, Maslahi Yako Ndiyo Lengo Letu', mwaka 2023 tumejipanga zaidi kuendelea kuwawezesha na kuwawakilisha watumiaji kwa weledi wa hali ya juu na tunategemea huduma bora zaidi kama watumiaji wa huduma za usafiri wa anga Tanzania." alisema.

Kyara alisema katika mwaka 2022 sekta ya usafiri wa anga iliendelea kuboreka baada ya kupitia katika kipindi kigumu kutokana na athari za mlipuko wa UVIKO -19, akikumbusha kuwa sekta hiyo ni miongoni mwa zilizoathirika kwa kiasi kikubwa na ugojnwa huo.

Alisema kwa wakati huu ambao TCAA-CCC inaelekea mwishoni mwa mwaka 2022 na kuanza mwaka mpya 2023, ni wakati sahihi wa kufanya tathmini ya yale yaliyotokea katika mwaka unaoisha na kubaini maeneo ambayo taasisi ilifanya vizuri na maeneo ambayo palijitokeza changamoto kwa lengo la kuweka mikakati ya kuboresha katika mwaka ujao.

"Katika mwaka huu tumeshuhudia kuongezeka kwa idadi ya watumiaji kwa maana ya abiria na mizigo bila kusahau miruko ya ndege nchini kwetu kulinganisha na kipindi kilichopita.

"Hatua hii inatokana na jitihada mbalimbali zilizofanywa na serikali ikiwamo kampeni iliyoendeshwa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kuvutia watalii nchini kwetu kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour.

"Jitihada nyingine zilizofanywa na serikali ni kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali. Ikumbukwe Sekta ya Usafiri wa Anga ni sekta muhimu ya kuchochea ukuaji wa sekta nyingine," alisema.

Kiongozi huyo alisema ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege unaohusisha njia za kurukia ndege na majengo ya abiria ni hatua zinazohitaji pongezi kubwa kwa serikali.

"Tukichukulia mfano mmoja, kuanza kwa ujenzi wa Kiwanja cha Kimataifa cha Msalato mkoani Dodoma, uwanja wa ndege ambao utaruhusu ndege kubwa zinazochukua abiria wengi kwa wakati mmoja, kutua kwenye mkoa huu wa Dodoma, ambao ndio makao makuu ya serikali na nchi yetu," alisema.

# Waziri amwaga vifaa tiba Hospitali ya Wilaya Magu

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mwanza na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja akiwa ameambatana na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Magu, amegawa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 14 kwa Hospitali ya Wilaya ya Magu pamoja na mitungi ya gesi 100 kwa wajawazito.

Akizungumza leo katika hafla ya ugawaji wa vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. 14,575,000 na mitungi ya gesi 100 kwenye hospitali hiyo, Masanja alisema vifaa hivyo vimetokana na mchango wake binafsi pamoja na Doris Mollel Foundation.

Masanja alisema vifaa tiba hivyo vitasaidia kuokoa maisha ya watoto waliozaliwa njiti na mitungi ya gesi itasaidia wajawazito kupunguza shughuli nzito za kutafuta nishati mbadala.

Pamoja na kugawa vifaa hivyo, Masanja aliwataka wajawazito kuhudhuria kliniki mara kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto anapokuwa tumboni.

Aidha, aliwataka wanawake wanachama wa UWT kumuunga mkono Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika jitihada anazozifanya za kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Magu, Dk. Maria Kapinga, alisema vifaa hivyo vitasaidia kunusuru maisha ya watoto wanaozaliwa kabla ya muda ( njiti).




Baadhi ya wafanyabiashara kutoka Mwalo wa Kibirizi mkoani Kigoma wakiendelea na biashara zao.**PICHA NA MPIGA PICHA WETU**

## Polisi yatangaza operesheni safisha

**Na Steven William,** MUHEZA

POLISI Wilaya ya Muheza, imetangaza operesheni ya 'safishasafisha' ya kuwaondoa mitaani watoto wanaofanya biashara ndogo, maarufu kama machinga, huku wakiwa na umri wa kwenda shule.

Kazi ya kuwaondoa mitaani watoto hao waliojiajiri au kuajiriwa na baadhi ya watu, ilitangazwa juzi na Mkuu wa Upelelezi wa makosa ya Jinai (OCCID), Charles Ntenga, baada ya kueleza kukerwa na hali hiyo.

"Tutawakamata watoto wote, ambao wanafanya biashara ya kuuza karanga na mayai mitaani, hasa ambao wana umri wa kuwa shuleni.

"Kuna watoto wadogo wanatakiwa kuwa shuleni, lakini wanafanya biashara ya kuzunguka mitaani, na wazazi wao wamewaachia wanafanya biashara hizo. Hilo ni kosa kisheria," alisema.

Ili kukabiliana na wimbi hilo la ajira ya watoto, Ntenga, alisema kuwa kuanzia mwezi Januari mwaka ujao, hataki kuona mtoto katika Wilaya hiyo, ambaye ana umri wa kwenda shule, anauza karanga na mayai.

Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, imeelekeza bayana muundo unaolenga kumpa mtoto kinga pamoja na viwango kwa ajili ya utoaji haki kwa watoto, na vilevile kanuni za kudhibiti ajira za watoto zimepewa nguvu zaidi katika sheria hiyo.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, watoto wana ruhusa ya kufanya kazi, baada ya kutimiza umri wa miaka 14, na kazi haipaswi kumzuia mtoto kuhudhuria masomo au kupata muda wa kujisomea na kupumzika.

Pamoja na mambo mengine, sheria hiyo inaelekeza kuwa yeyote anayewafanyisha kazi watoto kupita kiasi, au asiyewalipa ujira unaostahili, basi anavunja sheria hiyo.

# Viongozi wa mitaa wapewa somo utekelezaji wa miradi

**Na Magreth Lyimo**

MTAALAMU wa Mazingira kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendelo ya Makazi, Alpha Mangula amewataka viongozi wa serikali za mitaa ya Mapinduzi A, Mapinduzi B, Bihawana na Mkwawa jijini Dodoma kuyapa kipaumbele masuala ya kimazingira na kijamii katika utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP).

Mradi huo unaotekelezwa chini ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni wa miaka mitano kuanzia mwaka huu hadi 2027.

Wakati wa upembuzi yakinifu (screening) wa mitaa ya mfano jana, kiongozi huyo alisema: "Kazi hii inaitwa upembuzi yakinifu wa masuala ya kimazingira na kijamii ambapo hatua hii inasaidia kubaini changamoto za kimazingira na kijamii zinazoweza kujitokeza ili kutengeneza mpango mkakati utakaowezesha kukabiliana na changamoto hizo kabla ya kuanza kazi za uwandani".

Alieleza kuwa hiyo ni moja ya hatua muhimu ya mradi itakayowezesha kujua namna ya kutoa elimu na utekelezaji wa mradi pasipo kuathiri mazingira na maslahi mapana ya jamiii.

Alisema kikao hicho kinahusisha viongozi wa serikali za mitaa hiyo pamoja na Maofisa Maendeleo ya Jamii na Mazingira wa Jiji la Dodoma kwa kuwa wanawajua wananchi wao vizuri na wataibua changamoto za kimazingira na kijamii zilizopo katika mitaa yao ili kuwezesha utekelezaji wa mradi.

"Katika upembuzi huo vitu vinavyoangaliwa kwa ukaribu ni changamoto za kimazingira na kijamii katika hatua za uhamasishaji, upangaji shirikishi, upimaji shirikishi na ya mwisho ni hatua ya umilikishwaji," alisema Mangula.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mkwawa, Daudi Msaka alisema mradi huo utanufaisha mtaa wake kwa kuwa wananchi watapangiwa, watapimiwa na kumilikishwa ardhi huku masuala ya kimazingira na kijamii yakizingatiwa.

Aliishukuru serikali kwa kudhamiria kutekeleza mradi huo aliloueleza kuwa utawawezesha pia kupatikana barabara zitakazosaidia kuonekana na ni imani yake elimu watakayopewa itawasaidia kupata ushirikiano kutoka kwa jamii.

Hatua ya kufanya upembuzi yakinifu kwenye masuala ya kimazingira na kijamii katika mradi huo imefikiwa baada ya kuanza rasmi utekelezaji wa mradi waL-TIP ambapo katika awamu hii ya kwanza halmashauri 15 Tanzania zitafikiwa.

Mradi huo ni jitihada za serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kuimarisha miundombinu ya sekta ya ardhi na kuongeza usalama wa milki za ardhi kwa wanawake na wanaume.

# Mbaroni madai kulisha mifugo katika hifadhi

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

WATU sita ambao ni wakazi wa Emboret, wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuingiza na kulisha mifugo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Wanaoshikiliwa ni Muliyo Lekashu (25), Moringe Mpeleke (30), Sabaya Sumuni (38), Lemburis Roika (45), Terengo Kondeki (70) na Saruni Rosio (43). Baada ya kukamatwa kwa watuhumiwa hao, Kamanda wa Polisi, Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo nchini, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Simon Pasua, alisema jeshi hilo kupitia kikosi hicho kwa kushirikiana na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, mbali na kuwakamata watuhumiwa hao pia wamekamata ng'ombe 2,035, walioingizwa hifadhini kinyume cha sheria.

"Niwaombe wale wote wenye tabia za kuingiza mifugo ndani ya hifadhi waache mara moja kwani hatutasita kuikamata na kuitafisha kwa maslahi ya umma," alisema.

Alisema jeshi hilo linaendelea na upelelezi na mara baada ya kukamilisha upelelezi huo watuhumiwa watafikishwa katika vyombo vya sheria.

Aidha alitoa wito kwa wafugaji kufuata sheria za matumizi bora ya ardhi, kwa kuwa Jeshi la Polisi, halitofumbia macho vitendo vya uharibifu wa rasilimali za Taifa.

Aidha, Mhifadhi Mwandamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, William Maregesi, alisema wao kama wadau wakubwa wa uhifadhi, hawato sita kuwachukulia hatua wale wote watakao husika na uharibifu wa rasilimali za taifa.

Pia alisema kuwa wataendelea kuzilinda na kuhifadhi rasilimali za taifa kwa masilahi makubwa ya taifa na kuomba kila mmoja kuhakikisha anazilinda rasilimali hizo.

"Lakini mifugo yenu tukiikamata hatutasita kukamata kuwapiga faini na kuitaifisha kwa maslahi ya umma, sababu mnapoingiza hifadhini na kulisha mifugo yenu inasababisha uharibifu wa mazingira na kuhatarisha usalama wa wanyama pori," alisema.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Manyara, Peter Toima (katikati) akisalimiana na Mkuu wa Wilaya mstaafu wa Wilaya za Karatu na Sumbawanga, Mathew Sedoyeka (wa pili kulia) alipofanya ziara kwenye Wilaya ya Hanang' juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## WEO aamuru vijiji kulipa fidia wakulima

**Na Dege Masoli,** KILINDI

OFISA Mtendaji wa Kata ya Songe (WEO) wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, Ramadhan Dhahabu, ameamuru serikali za vijiji vya Vilindwa na Kwamba, kulipa gharama za wakulima waliopata hasara kwa kuandaa mashamba katika eneo la hifadhi ya Mlima Bokwa.

Viongozi wa serikali za vijiji hivyo wanatuhumiwa kuwapotosha wananchi kwamba eneo wanalofanya shughuli zao za kilimo, liko nje ya hifadhi ya mlima huo, hivyo wako sahihi kuendelea na uzalishaji wa mazao ya chakula.

Jana, Dhahabu alisema zaidi ya watu 600 waliokuwa wakifanya shughuli za kilimo katika mlima huo wameondolewa kwenye eneo hilo ambalo ni hifadhi.

"Nimeagiza wawalipe fidia hao wananchi kwa sababu ya upotoshaji wa viongozi ambao waliweka vibao vya mipaka ndani ya hifadhi, badala ya sehemu husika.

"Sisi tulibaini hilo tulipofanya ziara ya uhakiki na mkuu wa wilaya na kukuta watu wanapalilia mahindi ndani ya hifadhi." alisisitiza Dhahabu.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, katika hifadhi ya mlima huo kulikuwa na zaidi ya ekari 400 zilizokuwa zikilimwa kinyume na taratibu za uhifadhi.

Alipoulizwa Mwenyekiti Serikali ya Kijiji cha Kwamba, Abdi Makinda, kuhusu amri hiyo, alisema anashangazwa na uamuzi huo, kwa kuwa awali, Ofisa Mtendaji huyo alishindwa kufika kwenye mkutano wa hadhara aliouitisha kwa ajili ya kusikiliza malalamiko ya wananchi hao.

Aidha, Diwani wa Songe, Abubakari Makengwa, akizungumzia sakata hilo, alisema kinachoelezwa na serikali kinawezekana kuwa na ukweli, kwa kuwa wapo baadhi ya wakaidi.

# Waziri ataka wanafunzi kudumisha mila

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Madini, Dk.Steven Kiruswa, amewapa somo wanafunzi wa jamii ya kifugaji ya Kimasai wanaosoma vyuo vikuu na vyuo vya kati nchini, kuendelea kudumisha mila na desturi za kabila hilo ili kuweka na kuhifadhi kumbukumbu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Dk. Kiruswa, ambaye ni Mbunge wa Longido, alisema hayo jana jijini hapa wakati wa mahafali ya kwanza ya Jumuiya ya Wanafunzi wa Jamii ya Kifugaji (AMASA).

"Wanafunzi wangu hakikisheni mnaendeleza mila na desturi ambazo ni nzuri kwa ajili ya kuweka na kuhifadhi kumbukumbu kwa ajili ya vizazi vijavyo kwa kuwa kabila letu ni moja ya makabila nchini ambayo yanaendelea na utamaduni wake.


"Mila zote zina vipengele vizuri na vibaya lakini mimi nimewasihi na kuwasisitiza wanafunzi waendeleze kudumisha mambo mazuri ikiwamo mavazi yao ya asili, ujasiri na tabia ya kuheshimu watu katika jamii," alisema.

Hata hivyo, alisema katika safari yake ya elimu amefanikiwa kuandika hadithi za jamii ya kimasai kwa kuandika maandiko zaidi ya 200 na hadi sasa ameshatafsiri maandiko 70.

Pia alisema kuna umuhimu kwa jamii hiyo ya kifugaji kutoa fursa kwa watoto wa kike na wa kiume kupata elimu kwa kuwa awali walijikita zaidi kwenye suala la mila kuliko kuwapeleka wanafunzi shuleni. Mkurugenzi wa Mtandao wa Wafugaji Tanzania (TPCF), Joseph Parsambei, alisema wamefanikiwa kupiga hatua baada ya kuwekeza na kuwahamasisha wanafunzi wa kimasai kusoma ili kwenda kuikomboa jamii yao.

"Jamii za wafugaji kimsingi ni muhimu zipate elimu kama mpango mbadala kwa kuwa hali halisi ya ufugaji imekuwa ngumu kutokana na mazingira yenyewe,"alisema Parsambei.

Aidha, alisema moja ya matatizo yanayowakabili wamasai ni kuwapo kwa baadhi ya sheria ambazo haziungi mkono suala la ufugaji ikiwamo sera ya mifugo,wanyamapori na sheria ya wanyamapori na mashirika tumekuwa tukizungumzia jambo hili kila mara.



# Mbunge ataka wataje wanaume wanaowafanyia ukatili wanawake

**Na Mary Mosha,** SAME

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro, Zuena Bushiri, amewapa 'jeuri' wanawake wa Wilaya ya Same, kutoingia woga wa kuwafichua na kuwataja kwa majina waume zao ambao wamekuwa wakiwafanyia ukatili.

Bushiri aliwapa jeuri hiyo wanawake, alipokutana jana na wajumbe wa mkutano mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilaya za Same na Mwanga.

"Matukio ya ukatili yamekuwa yakiongezeka kila wakati. Kinamama msiogope wala kuwafumbia macho wale wote wanaofanya ukatili dhidi ya watoto na wanawake kwa sababu kufanya hivyo ni kuharibu kizazi cha baadaye. "Kila mtu anajua wanawake ni jeshi kubwa, na ndio wenye uchungu zaidi na watoto. Kila mmoja wetu ajenge urafiki na watoto wa kike na wa kiume ili waweze kuwaeleza yale wanayofanyiwa na watusaidie kuwafichua wahusika ili kukomesha matukio haya," alisema.

"Huko nyuma tulikuwa tukisikia watoto wa kike pekee, ndio walikuwa wakifanyiwa ukatili wa kijinsia, lakini kwa sasa hata watoto wa kiume, nao wamekuwa wakifanyiwa ukatili huo huo," aliongeza.

Ukatili wa kijinsia ni kitendo chochote ambacho kinaweza kusababisha madhara ya mwili,kingonoau kisaikolojia au mateso kwa wanajamii.

Mateso hayo ni pamoja na kutishiwa maisha, kunyimwa uhuru iwe hadharani au kwa kificho.

Moja ya ukatili, unaowatesa wanawake na watoto hivi sasa ni ubakaji na unajisi, ambavyo vyote ni udhalilishaji wa kingono na pia ni ukatili wa kijinsia.

Mwezi uliopita, Rais Samia Suluhu Hassan, alivunja ukimya kuhusu matukio hayo akieleza kusikitishwa kwake na kasi ya matukio ya ukatili wa kijinsia nchini.

Kutokana na kasi hiyo, Rais Samia aliagiza wataalamu wa maendeleo ya jamii, Mahakimu na wote wanaohusika na utoaji wa haki, kuhakikisha wanashughulikia upatikanaji wa haki kwa watoto na wanawake, ambao wanafanyiwa unyama huo.

## Tanga yasuasua uandikishaji shule awali

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

JIJI la Tanga limetajwa kuandikisha idadi ndogo ya wanafunzi wa shule za awali, tofauti na kiwango cha uandikishaji kilichopendekezwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Uandikishaji huo ndio utakaowapa fursa wanafunzi hao wa ngazi ya awali kuanza elimu yao Januari 7, mwakani.

Jana, Meya wa Halmashauri ya Jiji hilo, Abdulrahman Shiloow, alikiri kuwa kasi ya uandikishaji huo hairidhishi, kwa kuwa wako chini ya asilimia 50.

"Ukiacha malengo ya kitaifa, sisi Jiji la Tanga, tulijiwekea lengo la kuandikisha watoto kwa asilimia 100, lakini hadi sasa idadi hiyo haijafikiwa hata nusu yake.

"Hali hiyo inaashiria kuwa watoto wengi hawajaandikishwa. Tumefanya tathimini kwa uandikishaji watoto shule za awali, na mpaka sasa inaonyesha tumeandikisha watoto kwa asilimia 48 tu," alisema.

Kwa mujibu wa Shiloow, Jiji hili lilipanga kuandikisha wanafunzi zaidi ya 6, 400 lakini mpaka sasa hivi tumeandikisha watoto 3, 200.

"Maana yake, kuna watoto zaidi ya 3,200 hawajaandikishwa.Hivyo basi, tunawaomba na kuwasisitiza wazazi na walezi wa watoto wote, hata awe mlemavu naye ana haki, kwenda kuwaandikisha ili kutimiza malengo yetu katika jiji tuliyojiwekea," alisisitiza

Wanafunzi wa darasa la awali watakaoanza masomo mwaka 2023, ni wale wenye umri wa miaka mitano hadi sita.

Aidha, Meya huyo alisema mwisho wa uandikishaji huo ni Desemba 30 mwaka huu, huku akisisitiza mtoto aandikishwe shule iliyo karibu na eneo analoishi.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Babati Mjini Mkoani Manyara, Magdalena Uronu akisafisha mazingira kwenye Kata ya Maisaka kwa lengo la utunzaji wa mazingira juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Polisi yawaonya wavunja sheria

**Na Steven William,** TANGA

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Leopord Fungu, amewapa angalizo madereva wa mabasi makubwa ya abiria na magari madogo, wasimjaribu kwa kuvunja kwa makusudi sheria za usalama barabarani, akiwatangazia wajiandae kulipa faini kubwa kuliko wanavyotarajia.

Akizungumza jana na Nipashe, Fungu aliwaonya madereva wenye tabia ya kukimbia mwendo kasi barabarani, kwa kujaribu kuyapita magari mengine sehemu ambayo hairuhusiwi.

"Kikosi cha Polisi wa Usalama Barabarani, Mkoa wa Tanga, hivi sasa kimehamishia makazi barabara kuu ya Tanga/Dar/Arusha ili kutoa elimu kwa madereva wa mabasi na abiria wanaosafiri katika kipindi hiki cha kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka za Krismasi na mwaka mpya

"Lakini pia natoa onyo kwa madereva wanaotumia vilevi, ambao wanatoka Dar es Salaam kwenda Moshi (Kilimanjaro) wanasimamia Korogwe na Mji Mdogo wa Mombo wanakunywa bia. Sasa, tutawakamata na watakaobainika tutawafungia leseni zao za udereva kabisa," alisema.

Mbali na mwendokasi, aliwaonya pia madereva wa mabasi wenye tabia ya kuongea na simu ama kuchati kwa njia ya ujumbe mfupi (sms), huku wakiwa wanaendesha.

Alisema kutumia simu, wakati ni dereva wa chombo cha moto ni hatari, kwa kuwa anaweza kupoteza mwelekeo na kusababisha ajali inayogharimu maisha ya watu, kwa kusababisha vifo na ulemavu wa kudumu.

Kuhusu mabasi ya mikoani yanayobeba abiria 60 au zaidi, waache mara moja tabia hiyo, kwa kuwa kibano dhidi yao kinanukia, kwa vile watapigwa faini ama kufungiwa leseni zao.

Kwa abiria wanaosafiri na mabasi hayo, Fungu aliwasihi kuwa makini na matapeli kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka, kwa kuepuka kuuziwa na kupokea vyakula ndani ya basi na mtu wasiyemjua.

"Wakati huu ni hatari, wajanja wanauza au kutoa vyakula, ambavyo vinakuwa vimewekwa dawa za kulevya ili kupata fursa ya kuiba fedha ama mabegi ya abiria,"alisisitiza mkuu huyo.





## Wajasiriamali walia ugumu wa biashara

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

BAADHI ya wafanyabiashara Jijini hapa wamelalamikia hali ngumu ya biashara msimu huu wa kuelekea sikukuu za Krismasi na Mwaka mpya.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti jijini hapa, wafanyabiashara hao walikiri hali ngumu ya biashara kwenye msimu huu wa sikukuu.

Ally Adamu, mfanyabiashara wa nguo katika mtaa wa One Way, alisema msimu huu umekuwa tofauti na miaka ya nyuma ambapo wakati kama huu biashara huwa zimechangamka sana.

"Tulishazoea kutegemea msimu huu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kuwa ndio mkombozi wetu kibiashara lakini mpaka sasa matumaini yamefifia" alisema.

Adamu alisema wateja ni wachache na wengi wanataka bidhaa kwa bei ndogo jambo ambalo linawakatisha tamaa.

Alibanisha kuwa wanauza lakini kwa kiwango kidogo tofauti na mategemeo yao ya sikukuu kubwa kama hiyo.

Mfanyabiashara Alfred Chuwa, alisema hali ya biashara si nzuri lakini wana matumaini kwa siku zilizobaki huenda wateja wakajitokeza kununua bidhaa zao.

Alisema hali ya mabadiliko ya tabianchi imechangia kwa kiasi kikubwa kwa wakulima kukosa fedha za kununua mahitaji kama ambavyo imezoeleka katika sikukuu za nyuma.

Chuwa alisema kutokana na mvua zilizonyesha chini ya kiwango kwa msimu wa kilimo uliopita zimechangia hali ya mavuno kuwa chini na wakulima kukosa fedha za kujikimu kimaisha.

Aliongeza kuwa kundi la wakulima lilikuwa miongoni mwa wateja wao wakubwa wakati wa msimu wa sikukuu hizo.

Pia alisema wafanyabiashara wanategemea makundi mbalimbali ya uzalishaji ikitokea hali ngumu kwa upande mmoja inaathiri upande wa pili.

Mmoja wa wakazi wa jiji la Dodoma, Anna Petro, aliyekutwa eneo la duka akinunua mahitaji alidai kuwa wanafanya manunuzi kwa tahadhari ili kulinda fedha za ada za shule.

"Wazazi tunanunua mahitaji lakini tunabana fedha zingine kwa ajili ya kulipa ada za shule, kweli tunatamani kununua vitu vingi lakini kutokana na hilo lazima tuchukue tahadhari ya matumizi" alisema.

# Ashauri SACCOS kuanzisha miradi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, ameekitaka Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Ardhi (SACCOS) kuanzisha miradi itakayowanufaisha watumishi hata baada ya kustaafu.

Dk. Kijazi aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano mkuu wa pili wa Ardhi SACCOS, uliofanyika katika ukumbi wa Maktaba ya Taifa Tawi la Dodoma.

"Anzisheni miradi ya kiubunifu itakayosimamiwa na Ardhi SACCOS ambayo itawanufaisha watumishi wa sekta ya ardhi kwa kuwajengea uwezo wanachama wenu kumiliki viwanja na hata kuanzisha kampuni zitakazowasaidia pindi wakatapostaafu kazi," alisema.

Dk. Kijazi alisisitiza kuwa angependa kuona SACCOS hiyo inawanufaisha watumishi kwa kuwa na mikakati ya muda mrefu ya miaka mitano hadi 15 ili kuwaepusha kujiingiza kwenye shughuli zisizo za kimaadili wawapo kazini na hata baada ya kustaafu.

Pia aliwataka viongozi wa Ardhi SACCOS kukamilisha kwa haraka mradi wa viwanja wa Mapinduzi A ulioko jijini Dodoma kwa kuwa umechukua muda mrefu kukamilika, hivyo wakae na kutafutia ufumbuzi kikwazo cha kuchelewa kwa mradi huo.

Kadhalika, aliitaka SACCOS hiyo kuwakutanisha watumishi wa sekta ya ardhi katika fani zote za upimaji na ramani, mipango miji, uthamini wa mali na fidia na fani zingine zote ili kunufaika kwa kujiwezesha kiuchumi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ardhi SACCOS, anayemaliza muda wake, Wilson Luge, alisema amepokea kwa mikono miwili maelekezo, ushauri na maoni ya Katibu Mkuu na watashirikiana na menejimenti ya SACCOS hiyo kuyatekeleza.

"Mara baada ya mkutano huu kufungwa tutashirikiana na viongozi ambao watachaguliwa hivi karibuni kusimamia na kutekeleza maelekezo na ushauri alioutoa mgeni rasmi leo kwa Ardhi SACCOS kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake"alisema Luge.

Ardhi SACCOS ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Wizara ya Ardhi ambacho kilianzishwa rasmi mwaka 2020 na kina usajili na leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania na kina wanachama takribani 331 nchi nzima.



Baadhi ya wananchi wakipita kwenye mtaa wa One way Jijini Dodoma jana kwenye maduka mengi ya biashara mbalimbali wakiwa na pilikapilika za kutafuta mahitaji ya Sikukuu ya Krismas . **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwongozo madawati jinsia maeneo ya mikusanyiko ya watu waandaliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI inakamilisha mwongozo wa uanzishwaji wa madawati ya kijinsia katika maeneo ya mikusanyiko ya watu ikiwamo sokoni, hatua ambayo itasaidia kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Mwongozo huo pia utahusisha maeneo ya vituo vya usafirishaji abiria, mialo ya samaki na maeneo ya bandari.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Juma Samweli, alibainisha hayo juzi wakati akifungua kikao cha wadau chini ya uratibu wa wizara waliokutana jijini hapo kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo.

Alisema, kukamilika kwa mwongozo huo itakuwa ni muarobaini wa kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kwenye maeneo yaliyolengwa.

"Ili kazi hii iwe na umiliki wa sekta zote niwaagize wajumbe kutumia muda huu wa siku tatu kikamilifu kutafakari kwa kina na mtoke na mwongozo uliokamilika ninataka ifikapo Desemba 27, mwaka huu, uwasilishwe kwenye menejimenti ya wizara," alisema.

Serikali ikishirikiana na taasisi ya Equality for Growth (EFG) 2019 iliyotekeleza mradi "Mpe riziki si Matusi" ambao ulilenga kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia masokoni ulifikia masoko 15 ya mkoa wa Dar es Salaam na masoko sita kwa mkoa wa Shinyanga.

Aidha, Samweli alisema kuwa maeneo ya mikusanyiko ikiwemo masoko yamekuwa na malalamiko mengi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwa ni pamoja na lugha chafu za udhalilishaji na miundombinu mibovu ya utendaji kazi.

Pia kukosekana kwa usawa wa ushiriki wa Wanawake kwenye nafasi za uongozi na uamuzi, kutokuwa na mazingira salama ya watoto wanaofika kwenye maeneo hayo pamoja na kukosekana kwa madawati ya kijinsia yanayoweza kusaidia watu wanaofanyiwa ukatili.

Awali, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jinsia, Badru Abdulnuru, alisema kufikiwa kwa hatua ya mapitio ya mwongozo huo, ni hatua ya kujipongeza kwa kuwa kiu na hamu ya serikali ilikuwa ni kuona kuna kuwa na Mwongozo mahususi utakaosimamia suala la ukatili kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu.

Mratibu wa Mradi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Yohana Sekimweri, alisema wizara iliona ni busara kuwaita wadau kutoka sekta mbalimbali ili kupokea mchango wa mawazo ambayo yatasadia kuuboresha mwongozo ili uwe na sura ya kitaifa.

Matokeo ya mwongozo huo ni tafiti ya Afya ya Mtoto na Viashiria vya Malaria (TDHS-2015/16) vilionyesha kuwa asilimia 40 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 - 49 wameshawahi kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili na asilimia 17 wameshawahi kufanyiwa ukatili wa kingono.

Taarifa ya utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia ya mwaka 2017 kuhusu ukatili ulioko maeneo ya vituo vya usafiri, ilionyesha asilimia 77 ya wanawake wenye umri wa miaka 18-25 wamefanyiwa vitendo vya ukatili katika vituo vya usafiri.

Pia inaonyesha mwanamke mmoja kati ya wanawake watano wenye umri kuanzia miaka 15-49 katika mkoa wa Dar es Salam wamepitia ukatili wa kimwili, matumizi ya lugha zisizo sahihi na kejeli.





# Baraza laona mwanga mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Baraza la Vyama vya Siasa amewataka viongozi wa vyama vya siasa kuwa wavumilivu wakati serikali ikiendelea kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti ya kikosi kazi kwa ajili ya kujenga demokrasia na kuimarisha utawala bora.

Juma Ali Khatib alitoa rai hiyo jana visiwani hapa alipozungumza na waandishi wa habari, akisisitiza kuwa suala la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa ni miongoni mwa ajenda zilizozungumzwa na viongozi wa vyama vya siasa kwenye baraza hilo.

Alisema mikutano ndiyo uhai wa vyama vya siasa kwa kuwa inajenga mawasiliano na wanachama wao.

"Viongozi wa vyama vya siasa wenzagu, wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa tulifanya mkutano wa kujitambulisha na kufanya mazungumzo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ambaye ndiye mwenye dhamana ya vyama vya siasa na ametuhakikishia kuwa mambo mengi yaliyomo kwenye ripoti hiyo ya kikosi kazi yapo katika mchakato wa kukamilika, hivyo tumetakiwa tuwe na subira," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi wameonyesha dhamira ya kweli ya kuyapatia ufumbuzi mambo yote yaliyoibuliwa na kikosi kazi na kuona yanatekelezwa ikiwa ni sehemu ya nia ya kweli ya kukuza demokrasia katika mfumo wa vyama vingi.

Aliyataja baadhi ya mambo ambayo serikali ipo katika hatua za mwisho kutunga kanuni zake ni kuhusu mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa.

Akizungumzia kuhusu fedha za kuendesha Baraza la Vyama vya Siasa, Khatib alisema tayari yamekuwapo mawasiliano na serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama kuna mchakato unaendelea wa kuomba fedha Hazina na kutengewa fungu dogo kwa ajili ya Baraza la Vyama vya Siasa.

"Suala hili tumelizungumza, tunataka zitengwe fedha za kuendesha shughuli za baraza zisiingiliane na fedha za kawaida za matumizi ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa," alisema.

Aliongeza kuwa hivi karibuni kwanza baraza limekutana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene jijini Dar es Salaam kuzungumzia masuala hayo.

Pia alipongeza hatua zinazochukuliwa na Rais Samia kuimarisha na kuendeleza miradi mikubwa ya kitaifa ukiwa wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Mwalimu Nyerere huko Rufiji, Mkoa wa Pwani.

Alisema juhudi hizo zinaonyesha nia yake katika kulipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa nishati ya umeme kwa maendeleo ya taifa.



Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, Juma Ali Khatib akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## ZRB yajivunia mafanikio katika kukusanya mapato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mapato Yasiyo na Kodi Zanzibar, Said Ali Mohammed amesema malengo yaliyofikiwa katika kukusanya mapato, yanatokana na umoja uliopo baina ya wafanyabiashara na taasisi hiyo.

Mkurugenzi huyo alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wafanyabiashara kuelekea Wiki ya Mlipakodi huko Kiwengwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema bila kuwapo wafanyabiashara na kulipa kodi kwa wakati, kusingekuwa na Bodi ya Mapato (ZRB), hivyo kuna kila sababu kwa wafanyabiashara kushirikiana na taasisi hiyo.

Alisema lengo la ZRB siyo kumkomoa mfanyabiashara bali kukuza mapato kwa maendeleo ya Zanzibar katika kuboresha huduma zake ikiwamo miundombinu ya afya, barabara, maji safi na salama na shule.

Mkurugenzi huyo alisema ZRB inawajali wafanyabiashara kwa kuwasikiliza malalamiko yao katika kufikia malengo yao.

Alisema wafanyabiashara wote wanatakiwa kuwa kitu kimoja na siyo kuwaficha baadhi ya watu wasiolipa kodi na ndiyo maana kuna changamoto ya malalamiko kwa upande wao.

Wafanyabiashara hao walisema licha ya kukubali kulipa kodi, kuna kikwazo katika baadhi ya maeneo ikiwamo baadhi ya nyumba za kulala wageni hazijasajiliwa na hufanya kazi za kulaza wageni bila kutozwa kodi.

Hamza Mkonya Ali ni miongoni mwa wafanyabiashara hao, alisema wanapotembelewa na watendaji wa ZRB, baadhi ya watendaji hawana lugha nzuri kwa wateja wao, jambo ambalo hujenga uadui baina yao.

Mkurugenzi wa ZRB Kituo cha Mkoa wa Kaskazini, Ali Adinani alisema malengo ya kuanzishwa vituo hivyo kwnye mikoa ni kuwajali wafanyabiashara kuondokana na kero za kuzifuata huduma makao makuu ya ZRB huko Mazizini.

Alisema wako tayari kushirikiana na wafanyabiashara wa mkoa huo na kuzitatua kero zote za wafanyabiashara ili lengo la kukuza uchumi kufikiwa bila ya kukandamiza wafanyabiashara.

# 'Wasaidizi wa kisheria wapewe mafunzo kukabili ukatili kijinsia'

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Siti Abbas Ali amesema ipo haja wasaidizi wa sheria wa wilaya zote za Unguja na Pemba kupatiwa mafunzo kwa ajili ya kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wazee na watoto.

Aliwalisisha hoja hiyo jana mjini Zanzibar wakati akifungua mkutano wa siku moja wa mrejesho wa vikundi kazi vya wasaidizi wa sheria katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji kijinsia. Alisema wananchi wengi wana uelewa kuhusu udhalilishaji wa kijinsia na wana mwamko wa kuviripoti vitendo hivyo kwenye sehemu husika.

Alisema mwamkoa huo umetokana na juhudi za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika kutoa elimu kwa jamii na msaada wa kisheria.

Mkurugenzi huyo alisema wananchi wana haki ya kupewa elimu ya kujikinga na vitendo hivyo vya udhalilishaji na kuwataka wazee kukaa na watoto kuwaelimisha ili kuwatambua watakapopatwa na tatizo lolote ikiwamo udhalilishaji.

Alipongeza kazi nzuri inayofanywa na wasaidizi wa sheria na kuwaahidi kuzipatia ufumbuzi kero zinazowakabili ikiwamo posho ili kuwasaidia kujikimu kimaisha.

Pia aliitaka wizara kuhakikisha inawapatia elimu ya kisheria katika vipengele muhimu ili viwasaidie kuwa na utendaji mzuri wa kazi zao.

Wakiwasilisha ripoti ya mpango kazi kwa kipindi cha mwezi wa Oktoba hadi Desemba mwaka huu, baadhi ya wasaidizi wa sheria walisema pamoja na mipango waliyojiwekea kafika utekelezaji wao, kikwazo kilichopo ni migogoro katika ndoa, hali inayosababisha wimbi la talaka na watoto kudhalilishwa.

Bahari Issa ni miongoni mwa wasaidizi hao wa sheria aliyesema elimu ya ndoa inapaswa kutolewa kwa wanaojiandaa kufunga ndoa ili kupunguza talaka holela pamoja na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Aliomba kupatiwa posho kwa wakati pamoja na kuwataka masheha kusimamia suala la kupiga muziki hadi usiku wa manane kwa kuwa ni miongoni mwa vichocheo vya vitendo vya udhalilishaji.



## MAKABILA

UKURASA 16

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI DESEMBA 24, 2022



# HAMISA

YUKO WAPI ?

# Freddie Ndala Kasheba:-6

# Mchawi wa gitaa dazani, kombora, akalivunja, akazikwa nalo




**Na Adam Fungamwango**

LEO tunamalizia simulizi yetu kuhusu safari ya mwanamuziki nguli nchini Tanzania Freddie Ndala Kasheba aliyezaliwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo mwaka 1946 na kufariki nchini Tanzania Oktoba 22, 2004.

Kiongozi huyo, mtunzi na mpangaji wa muziki, anakumbukwa sana na mashabiki wa muziki nchini kwa staili yake aliyokuja nayo ya kupiga gitaa la nyuzi 12 ambalo lilibatizwa majina mengi kama dazani au kombora. Aina yake ya upigaji pia ilivutia watu wengi.

**Kifo na mazishi yake**

Mamia ya mashabiki wa muziki, viongozi, na wanamuziki wa bendi mbalimbali nchini walikusanyika nyumbani kwake maeneo ya Kinondoni Dar es Salaam. Pamoja na shughuli zingine za kumuombea zikiendelea, lakini pia bendi yake ya Ya Capital ilipiga muziki laivu nyumbani kwake kama ilivyo kwa taratibu na utamaduni wa Wakongomani.

Na wakati wa kuaga mwili wa marehemu, bendi hiyo maarufu mama Wazee Sugu walipiga wimbo uitwayo 'Takadiri.' Wimbo huo una mashairi yafuatayo.

"Makosa yangu sherie, nakuomba mpenzi mezea, sitayarudia tena, nafikiri nimeshaelewa ee, machozi yanidondoka oooo, chakula hakimezeki ninaposikia. Takadiri wangu nakupenda mpenzi tambua kwa asilimia tisini mapenzi yangu kuelekea kwako.

Nipeleke Namanga kwa kaka Bushiri, kupitia Longido kwa shangazi Mwajuma, machozi yanidondoka ooooo, chakula hakimezeki ninaposikia. Sitarudiarudia tena, nakuomba unisamehe, takadiri wangu nakuomba sahau sherie, machozi yanidondoka, mwili umepunguka mawazo."

Nakumbuka wakati mashabiki wa muziki wa dansi, wanamuziki, ndugu jamaa na marafiki wakiaga mwili wa Kasheba, wanamuziki wake wakiongozwa na King Kiki walikuwa wakipiga wimbo huo laivu, kiasi cha kuendelea kuzua simanzi kubwa.

Ndani ya sanduku la marehemu mlikuwa na gitaa. Mwamba alizikwa na gitaa lake. Na kwa mujibu wa wanamuziki wenzake walisema gitaa lile ni ule mpini wa gitaa la nyuzi dazeni alilolivunja kwenye mchuano kati ya bendi yake dhidi ya Maquis du Zaire miaka mingi iliyopita ukumbi wa Magomeni Kondoa.

Baada ya taratibu zote kufanyika, sanduku lililokuwa limembeba marehemu Kaseha lilipakizwa kwenye gari maalum kuelekea kwenye Makaburi ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Waombolezaji walipanda magari yao binafsi na mengine yale yaliyokodiwa kwa ajili ya kuelekea huko.

Safari iliishia Kinondoni, eneo maarufu liitwalo 'Mwembe Jini'. Huko nako mbali na wale waliotoka nyumbani kwa marehemu ambapo hakukuwa mbali sana na maeneo ya Kinondoni MK, kulikuwa na umati mwingine wa watu ambao walikuwa wametoka sehemu mbalimbali.

Huko nako watu walishuhudia kitu kingine ambacho ni nadra sana kukiona. Baada ya taratibu zote kufanyika, sanduku la marehemu liliteremshwa taratibu kaburini, huku wanamuziki watatu wakiongozwa na Kanku Kelly Nkashama wakipiga trumpet kwa staili ya huzuni.

Kulikuwa na jenereta ambayo mbali na kuzalisha umeme ambao ulitumika kwa mambo mbalimbali na kutangaza, lakini maiki hizo zilitumika kwa wapiga trumpet hizo ili waombolezaji wapate sauti kubwa na bora kutoka kwa maspika yaliyokuwa yamefungwa hapo.

Sauti za trumpet zilizokuwa zikipigwa makaburini hapo zilisababisha baadhi ya watu kuangua vilio.

Ilikuwa ni huzuni na simanzi kubwa kuzisikia, huku mwamba akishushwa kaburini kwenye nyumba yake ya milele.

Baada ya mwanamuziki Kanku, aliyewahi kuzipigia bendi za Maquiz Du Zaire na Kilimanjaro Connection na wenzake kumaliza kupuliza trumpet hizo, taratibu zingine za mazishi ziliendelea na baadaye ndugu jamaa, manilia na marafiki na hata taasisi mbalimbali ziliruhusiwa kuweka mashada ya maua kwenye kaburi lake.

Moja ya vitu vilivyoshangaza na kufurahisha wengi ni kwamba moja ya shada lilikuwa ni tumbo la gita lake alilolivunja kwenye mashindano.

Niliandika huko nyuma kuwa Kasheba alivunja mpini ukawa kwake, na tumbo la gita likawa upande wake.

Mpini ndiyo ule ambao walikuwa amelala nao kwenye jeneza au sanduku, na tumbo ya gita yaani upande wa nyuma ambao ulikuwa umevunjika, ulipambwa maua mazuri, yenye rangi mbalimbali na kuwekwa juu ya kaburi lake.

Kila kitu kilichofanywa kwenye mazishi hayo kiliashiria kuwa aliyefariki na anayezikwa ni mwanamuziki. Tuseme tu Kasheba alizikwa kimuziki.

## UDAKU TU



# Hamisa Mobetto yamkuta...

HATUA ya Hamisa Mobetto kukiri mahaba mazito kwa mshambuliaji matata wa Ufaransa, Kylian Mbappe huenda imeibua matatizo katika mahusiano yake ya kimapenzi.

Siku ya Jumatatu, mama huyo wa watoto wawili alidokeza kuwa anavutiwa na Mbappe na kudai kwamba anajifunza Kifaransa kwa ajili yake.

"À se damner (Nakukufia)," aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Najifunza kifaransa kwa ajili ya Mbappe," alieleza.

Mpenzi huyo wa zamani wa staa wa Bongo, Diamond Platnumz na ambaye ni mzazi mwenza wake aliambatanisha ujumbe huo na picha yake nzuri inayoonyesha akiwa ameshika tumbo lake huku akionekana mwenye mawazo.

Baadae siku ya Jumanne, mwanamitindo huyo alichapisha meme kueleza hali iliyoipata ndoa yake baada ya kukiri kumpenda Mbappe.

"Mume wangu kipenzi nywele zimefumuka kesho nataka kwenda kusuka naomba hela," mwanadada mmoja alimwandikia mumewe kwenye mtandao wa WhatsApp katika meme ambayo Mobetto alichapisha.

"Kamuombe Mbappe," Mumewe alijibu.

Katika maelezo ya meme hiyo, Mobetto aliweka wazi kuwa hali sawa na iliyompata mwanadada huyo imemkuta pia.

"Hali yangu kwa sasa yamenikuta," aliandika.

Mobetto ni miongoni tu mwa wanadada wengi ambao wametekwa moyo na mshambuliaji huyo wa PSG hasa baada ya mchezo wake mzuri katika fainali ya Kombe la Dunia ambayo ilifanyika siku ya Jumapili  Lusail, nchini Qatar.

Mapema mwaka huu, Hamisa Mobetto alitangaza wazi kwamba amezama kabisa kwenye dimbwi la mahaba.

Katika video aliyochapisha mitandaoni, mzazi mwenza huyo wa staa wa Bongo Diamond Platnumz alikiri mapenzi yake mazito kwa mpenzi wake mpya na kufichua kuwa yuko tayari kufunga ndoa naye.

"Hatimaye nimepata mtu. Nimepata mwanaume ambaye nahisi ni yeye nataka. Nahisi kama kwamba huyu ndiye mtu ningependa kushiriki maisha yangu yote naye," alisema kwa kujivunia na msisimko mkubwa.

Mobetto aligamba kwamba hatimaye amefanikiwa kupata mwanamume anayezungumza lugha ya mapenzi sawa na yeye.

"Kila kitu ni rahisi sana, kila kitu ni sawa" alisema.

Aidha alisema kuwa anatamani sana kuvishwa pete na mpenzi wake mpya na kuchukua majukumu ya mke.

"Nataka kuolewa naye. Nataka kuolewa na mtu wangu. Nataka kumpikia, nimuandalie nguo ili aende kazini. Je, hii ni ndoto? niamke? Ikiwa ni ndoto mtu tafadhali anichune niamke," alisema Mobetto.

Ingawa hakumtambulisha mpenziwe, Mobetto alimsifia sana na kusema kuwa yeye ndiye mume kamili kwake.

BASI SAWA

## Ray na Mwijaku vipi tena



DC wa Instagram, Mwijaku amemtaka muigizaji Vincent Kigosi 'Ray' kuipokea platfom mpya iitwayo Ticfy Prime na kufanya nayo kazi.

Mwijaku amesema, platfom hiyo itakuwa msaada kwa wasanii kunadi kazi zao za filamu mitandaoni lakini anafahamu wasanii wa Bongomuvi wanakuwa na tabia za kuharibu mambo kwa kuweka makundi.

"Nakufahamu vizuri Ray una tabia ya kususasusa, acha bwana. Nakufahamu Steven Nyerere, nakufahamu Hemed PHD na wenzenu, hamkawii kutengeneza magrupu na kuanza kusemasema labda kwa sababu hili halijaanzia kwenu.

"Hii ni yenu msije mkafanya kama mlivyofanya kwa mwekezaji fulani alikuja mpaka akaondoka," alisema Mwijaku.

## Linex aliuza viatu kupata nauli



MSANII wa Bongofleva, Linex amefunguka safari yake kutoka Kigoma kuja Dar es Salaam na treni iliishia Dodoma na ikamlazimu kuuza viatu vyake ili kupata nauli.

Alisema hiyo ilitokea baada ya kuchoka kumkimbia mkaguzi wa tiketi kwenye treni.

"Nilifika salama Dar es Salaam, lakini niliishia Dodoma na treni. Nakumbuka pale Dodoma nikauza mdundo wangu (viatu).

"Nakumbuka nilikuwa na raba moja kali sana nikamuuzia mwana elfu 25 na nikapanda basi kuja Dar," alisema Linex.



## DULLA MAKABILA MIKONONI MWA BASATA

BARAZA la Sanaa la Taifa (BASATA), limeeleza sababu ya kumuita msanii Dulla Makabila kuwa imetokana na maudhui ya kutumia kiongozi wa dini katika wimbo wake wa 'Pita Huku'

Wimbo huo wa Dulla unaonyesha vitendo viovu ambavyo watu wamekuwa wakivifanya visivyompendeza Mungu na kuwaelekeza njia ambayo watapaswa kuingia kutokana na wanayoyafanya.

Katibu Mtendaji wa Basata, Dk Kedmon Mapana, amesema wimbo huo ni mzuri ila kasoro yake ipo katika maudhui ya kumtumia kiongozi wa dini.

"Hatuna shida na wimbo kwani ni mzuri na una ujumbe mzuri kwa jamii, shida ipo katika kiongozi wa dini alipotumiwa, kwani watu wako very sensitive (makini) na dini zao na baadhi wameshalalamika kwa nini watumike wao.



## Wakazi aikubali singeli

RAPA wa Bongo, Wakazi ameibuka na kudai kuwa muziki mpya wa singeli unakuja kwa kasi kuchukua nafasi ya hip hop.

Wakazi amesema hayo kupitia ukurasa wake wa Instagram baada ya kupost ngoma mpya ya Dulla Makabila.

"Singeli ni ya kipekee na kitofauti, hivyo inaeleweka kama kuna watu hawatoipenda basi wana shida. Ila mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Singeli imepiga hatua kubwa na inafurahisha," aliandika Wakazi

"Wiki kadhaa zilizopita nilizungumza kwenye kongamano la Acces na nilisema kuwa nina amini kuwa singeli imechukua au inaenda kuchukua nafasi ya hip hop, kama muziki wa uhalisia wa maisha ya kila siku, na wenye maudhui ya kufikirisha.

"Meja Kunta, Sholo Mwamba, Kinata Mc na hadi Dula Makabila wanaibeba bendera vizuri."

## MITINDO YA DANSI NA MAANA YAKE

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA ya 1970 hadi mwishoni mwa 1990 kulikuwa na bendi nyingi za muziki wa dansi nchini.

Na hazikuwa ili mradi bendi tu, bali zilikuwa zikipiga muziki wa ushindani. Bendi moja ikitoa wimbo huu ukitrendi, nyingine nayo inajibu.

Ulikuwa ni wakati ambao hata soko la muziki wa dansi lilikuwa juu. Pamoja na kwamba kila bendi ilikuwa na jina rasmi, lakini pia ilikuwa kama kautaratibu fulani, bendi kuwa na mtindo.

Mfano Orchestra Safari Sound ilikuwa na mitindo mbalimbali kulingana na kiongozi anayeingia, kama vile 'Masantula, Ngoma ya Mpwita', baadaye 'Dukuduku' na mwishoni 'Ndekule.'

Maquis du Zaire walikuwa na mtindo tofauti nyakati tofauti kama vile 'Kamanyola Bila Jasho', 'Ogelea Piga Mbizi' 'Scania LBT 111','Zembwela' na 'Sendema.'

Kulikuwa na bendi ambazo majina ya mitindo yao ilikuwa haibadiliki. Leo tutaangalia maana ya majina ya baadhi ya mitindo ya bendi za muziki wa dansi.

**Msondo Ngoma**

Mtindo huu ulibuniwa na mwanamuziki wa zamani wa bendi hiyo, Muhidini Gurumo. Ulikuwa mtindo wa bendi iliyokuwa ikibadilika majina kutokana na wamiliki ambao ni taasisi ya wafanyakazi Tanzania.

Awali ilikujulikana na NUTA Jazz, baadaye JUWATA Jazz, halafu OTTU Jazz, mwishoni Msondo Ngoma Musica. Kote huko ilitumia mtindo wa Msondo Ngoma. Msondo ni ngoma ya kabila la Wazaramo ambayo hutumika kwa ajili ya kuwafunda wanawari.

**Sikinde Ngoma ya Ukae**



Gurumo alipoihama Msondo aliwaachia mtindo huo na kwenda kuasisi mtindo mwingine unaoitwa 'Sikinde Ngoma ya Ukae' kwenye bendi mpya iliyoanzishwa mwaka 1978, Orchestra Mlimani Park.

Kama kawaida, mtindo huu ulikuwa na jina la kabila lake la Kizaramo ukiwa na maana Sikinde ngoma ya nyumbani.

**Super Bomboka**

Huu ulikuwa mtindo wa bendi ya Dar International ya pili chini ya Marijani Rajab. Ilikuwa ni baada ya karibuni asilimia 80 ya wanamuziki kuondoka kwenye bendi huyo na kuasisi Orchestra Mlimani Park.

Kabla hawajaondoka, Marijani alikwaruzana na kiongozi wa bendi Abel Bathazar na kuamua kukaa pembeni, ingawa zipo taarifa kuwa alitimuliwa. Akajipumzisha bila kufanya shughuli yoyote ya muziki. Walipoondoka, mmiliki alimfuata Marijani ili achukue uongozi wa kuendeleza jahazi. Ndipo alipobuni mtindo huo wa Super Bomboka akiwa na maana bomu lililopasuka. Lilikuwa ni dongo.

**Watunjatanjata**

Ulikuwa ni mtindo wa bendi ya Washirika Tanzania Stars iliyokuwa ikimilikiwa na Muungano wa Vyama vya Ushirika Tanzania.

Iliondokea kuwa bendi maarufu sana kwenye miaka ya 1990. Kina Hamza Kalala, Adam Bakari na Eddy Sheggy walikaa na kubuni mtindo waliouita 'Watunjatanjata.' ilikuwa ni kifupi cha maneno, 'Watanzania Tuungane Kuondoa Njaa Tanzania.'

**Munisandesa**

Baadhi ya wanamuziki wa Washirika Watunjatanjata akiwemo Adam Bakari walitimuliwa kwenye bendi hiyo kwa utovu wa nidhamu, wakaenda kuanzisha bendi waliioiita MCA International. Haikudumu sana, lakini ilirekodi nyimbo zake ambazo zilitikisa sana na kuwa tishio kwa hata Njata yenyewe. Nyimbo hizo ni kama 'Kasoro Yangu Sijaijua', 'Baba na Mama', 'Moyo Wangu Sultani.'

Mtindo wao ulikuwa ni 'Munisandesa.' Ilikuwa ni kifupi cha maneno 'Muziki ni Safari Ndefu Sana.'

FILAMU

## Binti:: Mafataki acheni madenti wa kike

**Na Adam Fungamwango**

UKISOMESHA mtoto wa kike umesomesha familia nzima. Huu ni msemo maarufu sana nchini ukiwa na maana kuwa mtoto wa kike anapoelimika, inakuwa na faida kwa familia nzima kwa sababu yeye ndiye anayeitunza.

Atajua jinsi gani ya kutayarisha chakula bora, afya ya familia na vitu vingine. Leo tunaiangalia filamu moja iitwayo 'Binti Yangu wa Pekee'.

Ni filamu inayoonyesha vitendo vya kikatili vinavyofanywa kwa mtoto wa kike na baadhi ya vijana wa kiume, wakati mwingine hata familia.

Imechezwa na wasanii mbalimbali wakiongozwa na mzee fadhili Msisiri. Happy ni mwanafunzi wa sekondari kwenye shule moja kwenye moja ya kijiji hapa nchini. Huwa anakwenda shuleni akimpitia rafiki yake Angel. Siku moja wakati wanakwenda shuleni kiatu chake kikakatika, akakipeleka kwa fundi mmoja aitwaye Mnyeke.

Mnyele ni kijana muovu ambaye ana tabia ya kutembea na wasichana mbalimbali kijijini hapo. Akaona hiyo ndiyo fursa. Happy akamfuata fundi Mnyeke ili kuchukua kiatu chake. Fundi akamwambia akifuate kiatu chake jioni nyumbani kwake. Happy akawa na wasiwasi na hilo, lakini atafanyaje?

Jioni akaenda kwa Mnyeke. Kilimchokuta huko mwenyewe anajua. Mnyeke akatumia mwanya huo kumlaghai na kumlazimisha kufanya mapenzi.

Siku chache baadaye akaanza kuona mabadiliko kwenye mwili wake. Akamfuata Mnyeke na kumwambia tayari yeye ni mjamzito. Akakataa. Happy akamwambia hawezi kuruka, ni yeye ndiye alimtia ujauzito wakati ni mwanafunzi.

Dunia haina siri, si wazazi wa wote wawili waliojua hilo bali ni kijiji kizima. Mnyeke akalazimika kukimbia kwenye vijiji jirani akiogopa kukamatwa na kushtakiwa kwa kumpachika mimba denti.

Huku nyuma, ugomvi mkubwa kati ya wazazi wa pande zote mbili. Baba Happy anamlazimisha mkewe ampeleke binti nyumbani kwa wazazi wa Mnyeke wakamlee na mimba yake. Mzee Msisiri anampokea binti huyo.

Alikokimbilia, anakumbuka nyumba, alichoamua ni kwenda kwa mganga wa kienyeji ili wamfanyie dawa ya kutokamatwa hata kama akirejea kwao. Mganga akafanya kama




alivyoambiwa. Akamhakikishia hatokamatwa. Mnyeke akarejea nyumbani.

Wazazi wake wakashangaa na kushtuka kwa wakati mmoja. Akawaambia wasiwe na wasiwasi kwani ameshamaliza kila kitu.

Angel, mwanafunzi mwenzake Happy akamuona Mnyeke, akaenda moja kwa moja nyumbani kwa rafiki yake kwenda kumwambia mama yake habari za urejeo wa Mnyeke anayesakwa. Mama akaenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji na askari mgambo. Mnyeke akakamatwa kiulaini.

BONGO FLEVA

# 2022 mwaka wa historia kwa Nandy

Miongoni mwa mambo aliyofanya Nandy mwaka huu, ni kuachia EP yake 'Maturity' yenye nyimbo tano ambazo aliwashirikisha wasanii kama C Natty, Nviiri, Lody Music, Dulla Makabila na Oxlade wa Nigeria.

Hii ni EP ya tatu kwa Nandy ndani ya miaka miwili, alianza na 'Wanibariki EP' na 'Taste EP' ambazo zote zilitoka mwaka jana, ikiwa ni baada kutoa albamu moja, The African Princess (2018) chini ya Epic Records.

Na amefanya tena tamasha lake 'Nandy Festival' ingawa hakuweza kutumbuiza mikoa mingi kutokana na hali yake kiafya ambapo alikuwa ni mjamzito.

Hata hivyo, kuna ambayo amefanya au yamejiri katika maisha yake ya muziki na familia mwaka huu ikiwa ni mara ya kwanza, hivyo kuufanya mwaka 2022 kuwa wa kihistoria kwake. Haya ni miongoni mwa hayo.

Agosti Nandy alipokea cheti kutoka Recording Academy ambao ni waandaaji wa tuzo hizo za Grammy baada ya kushirikishwa kwenye wimbo, Melanin, wake Etana wa Jamaica kutokea kwenye albamu yake, 'Pamoja' ambayo ilishinda Grammy kama Best Reggae Album 2021.

Taratibu za Grammy ikiwa albamu itashinda tuzo watu walioshiriki kama wasanii na waandaaji hupewa cheti maalum cha kutambua mchango wao.

Hii ni mara ya kwanza kwa Nandy kupata heshima hiyo sawa na kundi la Sauti Sol kutokea Kenya ambao walishiriki kwenye albamu ya Burna Boy, Twice As Tall, iliyoshinda Grammy 2021 katika kipengele cha Best World Music Album.

Utakumbuka Grammy zinazotajwa kama tuzo kubwa zaidi za muziki duniani, zilianza kutolewa Mei 4, 1959, wakati huo zikifahamika kama Gramophone Awards, huku lengo lake kuu ni kutambua mafanikio katika tasnia ya muziki.

Hapo Julai 16, 2022 Nandy na Mchumba wake, Billnass walifunga ndoa katika kanisa la KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani Usharika wa Mbezi Beach, kisha harusi ikafanyika ukumbi wa Mlimani City na Mastaa kibao kuhudhuria.

Billnass alimchumbia rasmi Nandy Februari 20, 2022 alipomvisha pete ya uchumba mbele ya familia za pande zote mbili jijini Dar es Salaam ikiwa ni miaka sita ya mahusiano yao ingawa kuna kipindi waliachana na kurudiana.

Hii ni ndoa ya kwanza kwa wote wawili, hivyo ni historia ya isiyoweza kufutika kwao, ni mwaka ambao Nandy hawezi kusahau kiwepesi. Kwa mara kwanza wawili hao walikutana mwaka 2016 katika Chuo cha Biashara (CBE) Dar es Salaam ambapo alikuwa wanasoma.

Hata hivyo, mahusiano rasmi yalikuja kuanza kwenye tamasha la Fiesta mkoni Mbeya ingawa wenyewe hawakuweka wazi kwa wakati huo zaidi kuandamwa na tetesi za muda mrefu.

Baada ya kukosekana kwa miaka saba, mwaka huu zilirekejea Tuzo za Muziki Tanzania (TMA) ambazo zilitolewa Machi na Nandy alijizolewa nne akiwa ndiye msanii wa kike aliyeshinda tuzo nyingi zaidi.

Nandy alishinda vipengele vya Mwanamuzi Bora wa Kike wa Mwaka Bongofleva, Mwanamuzi Bora wa Kike wa Mwaka na Mwanamuzi Bora Chaguo la Mashabiki Kwenye Mitandao ya Kijamii – Mwanamke, huku wimbo wa Darassa 'Loyalty' aliyoshirikishwa ukishinda kama Wimbo Bora wa Kushirikiana.

Hii ni mara ya kwanza kwa Nandy kushinda tuzo za ndani (Tanzania) maana wakati anatoka kimuziki tayari tuzo za Kilimanjaro Tanzania Music Awards (KTMA) zilikuwa zimesimama.





# BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Orchestra Sikinde Original**

Bendi hii mpya ambayo imeanza kuleta upinzani kwa bendi kongwe, leo mkesho wa Krismasi itakesha katika ukumbi wa Mawasiliano Park, kesho siku ya Krismasi ipo ndani ya ukumbi wa Muungano mjini Morogoro.

Twanga Pepeta

Leo mkesha wa Krismasi wapo ndani ya ukumbi wa Pweza Beach Kigamboni, kesho sikukuu ya Krismasi watafanya vitu vyao ndani ya Andrews Lounge Sinza, Boxing Day wapo Escrow Pub Kigamboni.

**FM Academia**

Leo Jumamosi mkesha wa Krismasi, wapo ndani ya ukumbi wa Lion Garden Kwa Mbonde Kibaha mkoani Pwani, kesho siku ya Krismasi watafanya makamuzi katika ukumbi wa G7 Kifuru jijini Dar es Salaam.

**Waluguru Original**

Wakiwa na marafiki zao wa Town Classic Band, leo mkesha wa Krismasi wapo ndani ya ukumbi wa Terminal Pub Msamvu, mjini Morogoro, kesho siku ya Krismasi kwa pamoja watatoa burudani katika ukumbi wa F2 Florida.

**Special Band**

Chini Mwinjuma Muumin Kocha wa Dunia, kesho sikukuu ya Krismasi watakuwa bonanza Sky Motel mjini Bukoba na kisha usiku watafanya makamuzi ndani ya ukumbi wa Mint Club mjini humo mkoani Kagera.

**The Bogos Band**

Bendi hii inayoundwa na kundi kubwa la vijana ikiongozwa na Nyoshi El-Saadat, leo mkesha wa Krismasi wapo Kibozone Malamba Mawili, kesho sikukuu ya Krismasi itakinukisha katika ukumbi wa Kokoroko jijini Arusha.

**Tukuyu Sound Band**

Leo Jumamosi mkesha wa Krismasi wapo ndani ya ukumbi wa +255 Mikocheni, kesho Jumapili sikukuu ya Krismasi watakuwa Mawasiliano Park, Ubungo na Boxing Day wapo ndani ya ukumbi wa Liquid Kurasini.

**Kimokimo Band**

Wakiwa chini ya Khadija Mnoga 'Kimobitel', leo mkesho wa Krismasi wapo ndani ya ukumbi wa Florida eneo la Extertanal, kesho wapo ndani ya ukumbi wa Next Door Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani.

**Dar Musica Original**


Bendi hii inayoongozwa na Jado Field Force, leo mkesha wa Krismasi ipo ndani ya ukumbi wa Panandi Pananda Kiluvya kwa Komba, kesho sikukuu ya Krismasi ipo katika ukumbi wa Mtibu Motel Mboga Chalinze mkoani Pwani.

**Malaika Music Band**

Kundi hili linaloongozwa na mwimbaji nyota wa muziki wa dansi, Christian Bella, leo litafanya onyesho maalum la kuzindua ukumbi jijini Mwanza, kesho sikukuu ya Krismasi litakuwa ndani ya Desire Lounge mjini Geita.

**Msondo Ngoma**

Bendi hii kongwe, leo mkesha wa Krismasi ipo katika ukumbi wa Nefalanda Hotel Manzese Argentina, kesho sikukuu ya Krismasi ipo ndani ya ukumbi wa Dar  Safari Park Buza, Boxing Day wapo Gwambina Lounge Chang'ombe.



# ZARI: MIMI MREMBO KULIKO WOTE

KUELEKEA tamasha la Zari All White Party linalotarajiwa kufanyika wikiendi hii Kampala, Uganda, Zari The Bosslady ametoa neno.

Zari ambaye amezaa na Staa wa Bongofleva, Diamond Platnumz watoto wawili, Tiffah na Nillan, amedai yeye ndiye mrembo anayeiwakilisha vizuri Uganda.

"Mimi ndiye msichana mrembo Uganda wako naye, naiwakilisha Uganda vizuri sana." amesema Zari The Bosslady.

Zari ambaye kwa mujibu wa kura za mwaka 2017 kupitia Instagram na Facebook zilipigwa kura 809 huku akiwashinda Wema Sepetu aliyeshika namba mbili na Lulu Michael aliyeshika namba tatu, amesema bado ni mrembo.

Kimwana huyo amesema bado hajapata mrembo wa kushika nafasi yake, kwa kuwa anajua kutunza urembo wake ambao unamfanya aendelee kupendeza kila siku.

Itakumbukwa Zari The Bosslady, Mama wa watoto watano anayeishi Afrika Kusini na familia yake, ni mwanamke mwenye nguvu ya ushawishi Afrika Mashariki upande wa urembo na mitindo.

Ushawishi huo unaotokana na urembo wake, umemwezesha kujizolea followers wengi hadi kufikisha milioni 11.1 Instagram.

Zari ambaye ni mzazi mwenzake na msanii wa muziki wa kizazi kipya, Diamond Platnumz, amekuwa akiandaa tamasha hilo kila mwaka na amewahi kulifanya hapa nchini na kujizolea umaarufu mkubwa.

Mastaa wa muziki wa kizazi kipya ni miongoni mwa watu ambao wamekuwa wakifuatilia tamasha la kimwana huyo anayejigamba kuwa mrembo kuliko wote, huku likiwa na kiingilio kikubwa.

Wikiendi hii anatarajia kukusanya mastaa katika tamasha hilo litakalofanyika nyumbani kwao jijini Kampala Uganda litakalonogeshwa na wasanii mbalimbali kutoka ndani na nje ya Uganda.



# Vera afichua kuhusu ujauzito wake

NYOTA wa televisheni wa Kenya, Vera Sidika amefichua kuwa hakujijua kama amebeba ujauzito kwa kipindi cha miezi mitatu.

Akizungumza baada ya kutangaza ujauzito wa mtoto wake wa pili, mama huyo wa binti mmoja alisema kuwa alichukua hatua ya kufanya vipimo vya ujauzito baada ya kuhisi uchovu mkubwa usio wa kawaida.

Alieleza kwamba ilikuwa vigumu kwake kushuku ana mimba mapema kwa sababu alikuwa bado akimnyonyesha binti yake Asia Brown.

"Haikuwezekana kujua kwamba mimi ni mjamzito kwa vile sikuwa nikipata hedhi kwani nilikuwa nanyonyesha na huwa sipati dalili zozote za ujauzito hata kidogo. Ikiwa sikupima labda ningejua hadi miezi 5," alisema kupitia Instagram.

Alisema kuwa daktari wake alimshauri akome kumnyonyesha binti yake wakati ujauzito wake ukitimiza miezi minne hadi mitano.

"Sikuwahi kupata dalili za ujauzito nikiwa na ujauzito wa Asia. Sina dalili kabisa za ujauzito huu pia. Kusema kweli ni baraka sana kupata mimba laini. Nimebarikiwa," alisema.

Mwanasoshalaiti huyo pia alifichua kwamba anapanga kujifungua mtoto wake wa pili kwa njia ya upasuaji kama ilivyokuwa ujauzito wake wa kwanza.

"Ilikuwa laini sana mara ya mwisho. Ilikuwa vizuri. Nitaifanya tena," alisema.

Vera alitangaza ujauzito wa mtoto wake wa pili na mumewe Brown Mauzo siku ya Jumatatu kupitia ukurasa wake wa Instagram.



## R. Kelly apata mtoto akiwa jela

NYOTA wa muziki wa R&B wa Marekani, Robert Kelly (R.Kelly) na mchumba wake Joycelyn Savage wameripotiwa kupata mtoto wao wa kwanza pamoja.

Mtoto huyo wa kike waliempatia jina la Ava Lee Kelly, aliyetungwa kwa njia ya IVF.

IVF ni moja ya mbinu kadhaa zinazopatikana kusaidia watu wenye matatizo ya uzazi ya kutokushika ujauzito ambapo yai hutolewa kutoka kwenye ovari ya mwanamke na kurutubishwa na manii kwenye maabara.

Yai lililorutubishwa, linaloitwa kiinitete, hurudishwa kwenye tumbo la uzazi la mwanamke.

R.Kelly yupo jela akitumikia kifungo cha miaka 30 kwa kosa la kufanya ngono na wasichana wenye umri mdogo pamoja na kuwarekodi video.

## Ugonjwa waahirisha 'bethdei' ya Bahati

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Kelvin Mbuvi Kioko 'Bahati' wa nchini Kenya anapanga kusherehekea siku yake ya kuzaliwa Januari 28 mwaka ujao baada ya kushindwa kusherehekea mwaka huu kwa sababu ya kuugua.

Msanii huyo ambae ametimiza miaka 30 Desemba hii na mwenye watoto wanne, amesema pamoja na kwamba anaumwa, anaamini Januari 28 mwaka ujao atatimiza lengo lake la kusherehekea siku yake ya kuzaliwa.

"Nimetimiza miaka 30, lakini kwa bahati mbaya nimekuwa mgonjwa kwa wiki moja sasa, niko kwenye dozi, imebidi niahirishe sherehe yangu ya kuzaliwa hadi Januari 28 mwaka 2023," amesema Bahati.





## Nadia Mukami amtamani Fally Ipupa

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya Nadia Mukami anatamani kushirikisha mwimbaji wa muziki wa dansi Fally Ipupa, ili aweze kuwa na mafanikio makubwa katika miondoko hiyo ya kizazi kipya.

"Kwa sasa ninajiona wa kawaida sana, ila siku ya Mungu atakaponijalia nikaingia studio na kurekodi hata wimbo mmoja na Fally, nina uhakika nitakuwa nimetusua," amesema Nadia.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Nadia ameandika kuwa ndoto yake ya kufanya kolabo na mwimbaji huyo kutoka Congo DR ni ya muda mrefu na amekuwa akiiombea itimie.

Msanii huyo amesema anataka kuwa na mafanikio makubwa kimuziki na katu hawezi kubweteka hata kama atafanikiwa, badala yake ataongeza kasi ya kupata mafanikio zaidi.

MAKALA

# Viongozi watakiwa kunywa sumu kuokoa Ihefu, Ruaha

- MERICA yaja na mikakati kuokoa jahazi
- Dk. Mpango ataka viongozi wanaohusika wanywe sumu

Na Joseph Mwendapole



BONDE la Ihefu mkoani Mbeya na Mto Ruaha Mkuu ni miongoni mwa rasilimali muhimu kwa urithi wa taifa letu kutokana na umuhimu wake kwa upatikanaji wa maji lakini hivi sasa umevamiwa na shughuli za binadamu kiasi cha kuharibika.

Kwa mfano Bonde la Ihefu awali lilikuwa na ukubwa wa skwea kilomita 83 lakini kutokana na kuvamiwa na shughuli za binadamu ikiwemo kilimo cha umwagiliaji na ufugaji zimebaki skwea kilomita 10 tu mpaka kufikia mwaka huu.

Kwa mfano uchunguzi unaonyesha kwamba leo ni siku ya 136 mto Ruaha ukiwa haujatiririsha maji jambo ambalo si la kawaida kuwahi kutokea kwa miongo mingi iliyopita.

Hii inatoa ishara mbaya sana kwa vizazi vijavyo kwamba iwapo serikali haitachukua hatua za dharura kuokoa hali hii kuna uwezekano vizazi vijavyo vikakosa huduma muhimu ya maji ambayo yanategemewa kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji hususan viwandani.

Baada ya kuona hali inazidi kuwa mbaya, waandishi wa habari wameamua kuonyesha uzalendo kwa kuanzisha kampeni ya kuokoa bonde la Ihefu na Mto Ruaha ili liweze kutiririsha maji kama ilivyokuwa zamani.

Waandishi wameaanzisha Chama cha Kutetea Mazingira na Rasilimali (MERICA), ambacho kiliandaa kongamano la mazingira mkoani Iringa lililofunguliwa na Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango mapema wiki hii.

Miongoni mwa aliyoyasema Dk. Mpango wakati wa ufunguzi wa mkutano huo ni kuhusika kwa baadhi ya viongozi kwenye uharibifu wa mazingira hali inayowafanya wapate kigugumizi kutekeleza maagizo ya serikali.

Alisema ametoa maagizo mara kadhaa kuhusu utekelezaji wa maagizo ya kuokoa bonde la Ihefu na Mto Ruaha lakini kwa muda mrefu hakuna kinachotekelezeka.

"Bahati mbaya sana kuna kundi la baadhi ya viongozi ambao kwa maslahi binafsi wanachangia sana kwenye uharibifu wa mazingira, mimi siamini kwamba wale wanaoswaga ng'ombe wamevaa matairi ndio wenye ng'ombe 3,000 na kuendelea.

"Wala siamini kwamba wakulima maskini ninaowajua kwamba ndio wenye mashamba makubwa wenye matrekta yanayoziba mito yetu na kupeleka kwenye mashamba yao, hawa ndio watu ninaosema wanywe sumu wakaue maslahi yao binafsi ili mazingira ya taifa letu yapone," anasema Dk. Mpango.

Anasema lazima iwepo mikakati ya kuokoa mito yote hususan ile ya kimkakati kama Ruaha Mkuu na kuongeze kuwa mazingira yameshaharibiwa na yenyewe yameamua kulipa kisasi na ndiyo sababu hivi sasa nchi inahangaika na uhaba wa mvua na maji.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Deodatus Balile, anasema mwaka 1974 bakuli la ardhi oevu la Ihefu lilikuwa na ukubwa wa skwea kilomita 83 lakini mpaka sasa limepungua zimebakia skwea kilomita 10.

Anasema limepungua kutokana na shughuli za kilimo na ufugaji ambapo wakulima hao na wafugaji wameendelea kuliz-ingira na kufanya shughuli zao kama kawaida.

"Ng'ombe mmoja akikamatwa faini yake ni Sh 100,000 lakini ikitolewa namba ya malipo mtu anaweza kulipa ndani ya sekunde 20 hata yangekuwa mamilioni lakini ng'ombe wakikamatwa wakisema wawanadi wahusika wanakamatwa na unakuta Naibu Waziri anapiga simu ng'ombe waachiwe," alisema Balile

"Hawa ng'ombe wakikanyaga bonde la Ihefu inamaana ile ardhi oevu wanaikandamiza inakuwa ngumu kama bati na mvua ikinyesha maji hayaingii ardhini na badala yake yanapita zake kwa hiyo bonde hili ambalo linapokea maji kwenye mito 26 na kutiririsha maji kwenda Ruaha Mkuu linakosa sehemu ya kuhifadhi maji," alisema

Anasema kwa mara ya kwanza mto Ruaha ulikauka mwaka 1994 na mwaka 1995 ukatokea mgao wa umeme hali iliyosababisha serikali kuanza kununua Megawati 100 kutoka kampuni binafsi ya uzalisha umeme ya IPTL.

Anasema mwaka 2005 mto huo ulikauka kwa mara ya pili na 2006 serikali iliamua kuanza kununua umeme kwenye makampuni binafsi ya Dowans na Richmond hali ambayo ilisababisha kashfa kubwa ndani ya serikali.

"Mwaka 2008 serikali iliamua kutoa notisi ya serikali namba 28 kwamba iongeze mbuga ya Ruaha kulinda vyanzo vya maji na kweli maji yalianza kuongezeka na vigingi havikuwekwa kwa miaka 14 na mwaka huu ndipo vimeanza kuwekwa vimefikia 45," anasema Balile.

"Kwa masikitiko makubwa kuna Ranchi ya Usangu ambayo ukiuliza watu wanasema hawajui nani anaimiliki lakini sisi tunafanya habari za uchunguzi inamilikiwa na familia 12 wakiwemo vigogo serikalini na majina tunayo tutakukabidhi," alisema

Godwell Ole Meleing'ati ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi na Kamanda wa Uhifadhi Ruaha, alisema changamoto ya matumizi mbalimbali yaliyokinzana na yasiyo rafiki kwa mazingira yaliathiri na kusababisha kukauka kwa mto Ruaha.

Anasema mwaka 1994 Mto Great Ruaha ulikauka kabisa na kwa mara ya kwanza tangu kuwepo kwake na mwaka 1995- hali ilizidi kuwa mbaya na kuathiri uzalishaji wa umeme na mwaka 1998 - Serikali iliingilia kati na kuamua kuweka eneo la usangu mashariki kuwa sehemu ya pori la akiba la Usangu ,wavuvi na wafugaji waliondolewa eneo hilo.

Anasema mwaka 2006 hali ilikuwa mbaya zaidi baada ya wafugaji na kilimo kushamiri Serikali ilifanya operesheni ya kuhamisha mifugo yote kutoka Usangu kwenda kwenye maeneo mengine na mwaka 2008- Pori la akiba la Usangu na baadhi ya maeneo ya vijiji yaliongezwa kuwa sehemu ya Hifadhi ya Ruaha, ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji za ardhi oevu ya Usangu na Mto Great Ruaha.

Anasema Bonde la Usangu lina zaidi ya maeneo ya umwagiliaji 408 na kati ya hayo 2.7% zimeboreshwa, asilimia 18 zimeboreshwa kidogo, 23.3% ni maeneo ya umwagiliaji wa asili/kienyeji na 55.4% ya maeneo hayo hayana vibali vya matumizi ya maji.

Kuhusu nini kifanyike kuokoa hali hiyo anasema lazima kukamilisha zoezi la mipaka ya Hifadhi ya Ruaha kwa kuweka alama, tathmini ya mali, malipo ya fidia, kuhama, kuondoa wavamizi wanaofanya shughuli ndani ya Hifadhi ya Ruaha kulingana na notisi ya serikali namba na marekebisho, kuondolewa kwa idadi kubwa ya mifugo katika Bonde la Usangu, mifugo imezidi katika bonde la Usangu (Zaidi ya 300,000), uwezo wa bonde ni mifugo 65,000.

Anasema kuna umuhimu wa kutekeleza mkakati ya usimamizi wa vyanzo vya maji vya Mto

Ruaha Mkuu, kutambua vyanzo vyote vya maji, kusitisha uchepushaji wa maji , kubomoa kuta na kuondoa mabanio, kusitisha kilimo kiholela, tathmini ya matumizi ya maji kwenye mashamba makubwa, upandaji wa miti, kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi, kujenga miundombinu ya kuwezesha wanyama kupata maji na mbinu bora za kuwezesha Mto Great Ruaha kutiririsha maji, ujenzi wa kingo Ngiriama na mabwawa na visima vifupi na virefu.

# VIBOKO WANAPOGEUKA KIPUSA DUNIANI

**Na Mwandishi Wetu**

VIKWAZO vikali vilivyowekwa katika usafirishaji wa pembe za ndovu, sasa wafanyabiashara wamegeukia wanyama aina ya kiboko kwa kuuza kwa faida kubwa mazao yao ikiwamo meno yao.

Kutokana na kukua kwa kasi kwa biashara hiyo kimataifa, wanaharakati wa wanyamapori wanaonya kuwa na uwezekano wa kuibuka kwa madhara makubwa kwa spishi ya wanyama hao ambayo tayari imeorodheshwa iko katika hatari ya kutoweka.

Baada ya Uingereza na mataifa mengine kutangaza kupiga marufuku biashara ya pembe za ndovu, shirika la usaidizi la ustawi wa wanyama liliamua kufanya uchunguzi katika soko la mtandaoni kujua nini hatma ya zuio hilo.

Katika utafiti huo waligundua kuna ongezeko la biashara ya meno ya kiboko ndani ya mwezi mmoja.

"Tuligundua ongezeko la biashara ya meno ya kiboko nchini Uingereza ndani ya mwezi mmoja baada ya kutangazwa kwa marufuku ya pembe za ndovu kuanzishwa," anasema Frankie Osuch, mwandishi mkuu wa ripoti iliyotolewa na Born Free Septemba, mwaka huu.

Watafiti wanasema biashara hiyo ilikuwa wazi tangu mwaka 1989, wakati marufuku ya kimataifa ya biashara ya pembe za ndovu ilikubaliwa kwa mara ya kwanza, huku serikali zikileta hatua mpya za kuimarisha marufuku hiyo.

Kama ilivyo pembe za ndovu, meno ya kiboko nayo mara nyingi hutumiwa kwa michongo ya mapambo, lakini ni ya bei nafuu na rahisi kupatikana.

Nyama ya kiboko bado inaweza kuuzwa chini ya Mkataba wa Biashara ya Kimataifa katika Viumbe vilivyo Hatarini Kutoweka (CITES), ingawa mauzo yote ya kimataifa yanahitaji kibali cha kuuza nje.

Inakadiriwa kuwa kati ya mwaka 1975, wakati rekodi za CITES zilianza, na 2017, kilo 770,000 za meno ya kiboko ziliuzwa kisheria. Lakini kuna biashara haramu ilifanyika.

Mnamo 2020, meno ya kiboko yalikuwa kati ya sehemu za maghafi kutoka kwa mamalia ambazo mara nyingi hukamatwa katika nchi za Ulaya.

"Kuna visa vya mbwa wanaonusa kubaini meno ya kiboko katika viwanja tofauti vya ndege barani Afrika siku hizi, na imegunduliwa wengi hawakukamatwa," anasema.

Philip Muruthy, makamu wa rais wa Shirika la Wanyamapori la Afrika.



**"Tuligundua ongezeko la biashara ya meno ya kiboko nchini Uingereza ndani ya mwezi mmoja baada ya kutangazwa kwa marufuku ya pembe za ndovu kuanzishwa," anasema Frankie Osuch, mwandishi mkuu wa ripoti iliyotolewa na Born Free Septemba, mwaka huu.**



Utafiti wa Muungano wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) unasema 2016 ulikadiria kuwa idadi ya kiboko duniani kote ilikuwa kati ya 115,000 na 130,000. Lakini ilishuka kwa asilimia 30 ilipofika 1994.

Nchi 10 za Afrika Magharibi na Kati zinasema kumeendelea kupungua kwa kasi kwa idadi ya wanyama hao, kutokana na ujangili na uharibifu wa ardhi.

Walipendekeza kupigwa marufuku kabisa kwa biashara hiyo katika maandalizi ya mkutano wa CITES huko Panama mwezi uliopita.

Hata hivyo, hatua hiyo ingewezekana chini ya sheria za CITES ikiwa kungekuwa na kupungua kwa zaidi ya asilimia 50 ya idadi ya kiboko katika miaka 10 iliyopita, na uchambuzi wa IUCN haukuunga mkono hitimisho hilo.

# Simulizi aliyerudi CCM figisu alizofanyiwa

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa**
Korogwe

"KAMA nitawakwaza naomba mnisamehe, nilihamia CHADEMA, kutokana na udhaifu wa baadhi ya viongozi wa CCM wa Kata ya Kwashemshi. Chama kisimshike mtu kishike maoni ya wananchi."

Ndivyo anavyoanza kusema, aliyekuwa Diwani wa Kwashemshi, Korogwe Vijijini mkoani Tanga, Twahiru Salehe, wakati akitangaza kurudi CCM katika mkutano maalum, wiki iliyopita.

Mkutano huo ulikuwa ni wa mapokezi ya Mwenyekiti mpya wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Taifa, Mary Chatanda aliyefika nyumbani kwao Korogwe kwa mara ya kwanza tangu achaguliwe kushika nafasi hiyo.

Katika mkutano huo, baadhi ya wanachama wa upinzani walitangaza kujiunga na CCM akiwamo diwani huyo ambaye alieleza alikuwa mwanachama anayeipenda CCM, lakini akafanyiwa 'figisu', akalazimika kuondoka.

"Mtindo wa baadhi ya viongozi wa CCM kutofuata maoni ya wananchi, unasababisha chama kupoteza watu ambao wanapendwa na wapigakura kama ilivyotokea kwenye kata yetu ya Kwashemsi," anasema Salehe.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Taifa, Mary Chatanda, akivishwa skafu alipowasili Korogwe na kuhutubia mkutano na kuwapokea baadhi ya wanasiasa waliorejea CCM. **PICHA: SABATO KASIKA.**

**KISA KILIVYO**

Anasema yeye alikuwa kada wa CCM tangu mwaka 2010 wakati akisoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, lakini akajikuta akilazimika kuhamia CHADEMA Juni mwaka 2020 wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu.

"Kwa nini nilitoka kwenye chama ninachokipenda kutoka moyoni na kwenda CHADEMA, hii ni kwa sababu ya udhaifu wa baadhi ya viongozi wa CCM. Naomba kama nitawakwaza, mnisamehe," anasema.

Mwanasiasa huyo kijana, anafafanua kuwa viongozi walibeba watu wao katika uchaguzi huo na kusababisha aondoke kwenda kutafuta kuwatumikia wananchi kupitia chama kingine na akashinda.

"Ili kosa la aina hii lisijirudie kwenye kata nyingine, chama kisiwe na mtu, kishike maoni ya wananchi, kama kingeshika maoni ya wananchi,mimi nisingehamia CHADEMA. Na huo ndio ukweli, na kwa kuwa nimeapa kuzungumza, ukweli lazima niseme hata kama unauma," anasema.

Huku akishangiliwa na makada wa CCM katika mkutano huo, anatoa sababu za kumrudisha CCM kuwa ni kutokana na jinsi serikali inavyofanya kazi kwa bidii ya kuwaletea wananchi maendeleo.

"Kwa miaka miwili ambayo nimekaaa madarakani kila nilichokuwa nikiomba serikalini, kwa ajili ya maendeleo ya wakazi wa kata yetu, kimetekelezwa ikiwamo huduma ya maji, hivyo ni vyema niungane nayo," anasema.

Selehe anaongeza; "Mwanamke unayempenda usipomwambia ukweli maana yake unampotosha. Kwa kuwa chama hiki nakipenda kutoka moyoni, lazima niseme ukweli kwa viongozi waliopo hapa, ili tukitoka twende kuanza ukurasa mpya na kuendeleza gurudumu la kuwapambania wananchi na kuwaletea maendeleo. Tuache udhaifu."

**AUNGWA MKONO**

Mwenyekiti wa UWT Taifa Mary Chatanda, anaunga mkono kauli ya diwani huyo aliyerejea CCM na kuwataka viongozi wawachie kazi wanachama wachague watu wanaotaka wawaongoze.

"Viongozi acheni kubeba wagombea, waachieni wanachama wenyewe wachague kiongozi ambaye wanapenda awaongoze, msisababishe watu kuchukia chama kwa maslahi yenu," anasema Mary.

Anafafanua kuwa mgombea ambaye ni chaguo la wapigakura, ni vyema asifanyiwe mizengwe na viongozi, kwa kuwa ndiye chaguo lao, na kwamba wanajua kwa nini wanataka awaongoze.

Anaongeza kuwa hatua hiyo ya viongozi kutoingilia uchaguzi na kuweka watu wao, inaimarisha umoja ndani ya chama na hata kwenye jumuiya zake, kwa kuwa CCM inaamini kwamba umoja ni ushindi.

"Ni vyema makosa kama haya yaliyosababisha Salehe kukimbilia CHADEMA yasijirudie tena. Viongozi wetu zingatieni maoni ya wengi, yaani wapigakura wanamtaka nani ndiye apendekezwe," anasema.

> **"Kwa nini nilitoka kwenye chama ninachokipenda kutoka moyoni na kwenda CHADEMA, hii ni kwa sababu ya udhaifu wa baadhi ya viongozi wa CCM. Naomba kama nitawakwaza, mnisamehe," anasema.**

Aidha, mwenyekiti huyo anagusia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 na kusema wanawake wana jambo lao mwaka huo, na kwamba ili litimie, wanapaswa kuwa kitu kimoja, kwa kuwa umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

"Kwanza kabisa tuvunje makundi, uchaguzi umekwisha na sasa ni kazi tu, hivyo ili jambo letu litimie, hatuna budi kuwa wamoja na kuacha vikao vya kujadili watu bali tujadili maendeleo," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, wakishirikiana, wanaweza kurudisha chama na jumuiya zake kwenye enzi za TANU, kwa kuwa enzi hizo kila mwanachama aliwajibika kwenye nafasi yake na kuifanya UWT kuwa imara.

Anasema, viongozi wa umoja huo na wanachama wakiwa kitu kimoja watamsaidia mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan kutekeleza majukumu yake kikamilifu, kwa kuwa wanawake ni jeshi kubwa.

**MIRADI, WANACHAMA**

Mwenyekiti huyo anahimiza umoja huo kuwa na miradi ya maendeleo, ili kuuwezesha kujitegemea na hata kusaidia chama kushiriki kukamilifu katika uchaguzi wa mwaka 2024/2025 na kuibuka na ushindi wa kishindo.

"Wakati wa mkutano wa uchaguzi wetu, Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan alieleza kutoridhishwa na kasi ya kujiunga kwa wanachama wa UWT na uendeshaji wa miradi yetu ya kiuchumi," anasema.

Anasema, Mwenyekiti wa CCM Taifa anawaelekeza kufanya miradi mikubwa itakayoipa UWT nguvu ya kiuchumi na kuongeza wanachama, na kwamba atahakikisha maelekezo hayo yanatekelezwa kwa ngazi zote.

"Tayari UWT mkoa wa Tanga umeshaingiza wanachama wapya 2,547, mikoa mingine iige mfano huo, lakini pia suala la miradi yetu ni kweli kwamba, mingi ni ya vibanda, mashine za kusaga na mingine midogo ambayo haijatupa nguvu ya kiuchumi, hivyo kuanzia 2023 tutaongeza mingine," anasema.

Anasema chini ya uongozi wake atahakikisha UWT haijisahau badala yake watachapa kazi usiku na mchana ili kuhakikisha umoja huo unakuwa na wanachama wengi na pia nguvu ya kiuchumi.

"Jambo la muhimu ni kusimamia miradi iliyopo na kuongeza mingine. Mfano, UWT Wilaya ya Handeni wamepata mizinga 50 ya nyuki kutoka Shamba la Nyuki la Mwambao waanzishe mradi wa kufuga nyuki," anasema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Maendeleo kutoka miaka 10 ya Uhuru, hadi ilikogota leo kwenye miaka 61

## ●Pantoni Rufiji hadi daraja, mabehewa ya 'uswazi', hadi digitali...

**Na Adam Fungamwango**

NAKUMBUKA mzee wetu Alhaj Ali Hassan Mwinyi, alipokuwa kwenye uongozi wa Taifa, alikuwa mtu wa wosia sana na staili yake alitumia ama lugha ya kiswahili ambayo unaweza kusema ni sebuleni kwake, au anatumia misemo ambayo ukiunganisha ujumbe unajitosheleza hauachi hata pengo.

Alikwishatutamkia 'kila zama na azma zake'. Nani anaweza kubisha hilo? Hebu jikumbushe wewe, mzee wa leo mkaka ambaye utotoni kwako kidali pooh! ndiyo ilikuwa mpango mzima, huku dada yako ambaye leo ameingia kwenye zama za ubibi, humwambii kitu kwa 'babua ea.' Thubutu, leo hii umwambie mtoto wa leo akacheze michezo hiyo, utazua gumzo na kupondwa mpaka basi na kali zaidi wengine watashangaa na kukuuliza 'ndiyo nini hiyo?'

Vivyo hivyo, serikalini kwa awamu na muda husika, huwa kuna mahitaji yake, hasa ya maendeleo na aina fulani ya maendeleo hayo huibuka kipindi fulani yuko kwenye kiti; yaleyale ya kila zama na azma zake.

Naam! Lazima nikiri katika safari za awamu hizo mbalimbali, tunapoeleza kukomboa sekta ya usafiri na miundombinu, mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, zama na azma zake, ziliangukia hapo, sambamba na afya akizindua Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Nikunong'oneze kidogo, ile barabara iliyofungua ukanda wa Tabora hadi Kigoma, mabasi yanakatiza tu leo hii, akiipigania kwa nguvu zote.

Kutoka Masasi hadi Tunduru, kutokezea Namtumbo Ruvuma ni kichekesho kidogo mabasi leo yanakatiza kilaini, thubutu ungekuja na msamiati huo siku zile anaingia madarakani. Ushahidi ninao!

Nenda pale Temeke Sudan, Dar es Salaam, mabasi kibao kwenda Tunduru hadi Songea kupitia njia hiyo ya Masasi. Jamani! Inanirudisha nyuma tena zama zile, mzee Mwinyi akahamisha barabara ya mlima Lukumburu, sasa leo hii waendao Songea kupitia Njombe, mambo safi tu. Maana yake nini? Kuna kazi inafanyika. Tusiwe wataalamu wa kubeza tu.

Hebu niwape mchapo kidogo kwa kionjo cha safari ya Kusini zama hizo. Ukitoka Dar es Salaam, na ukafika kwenye kivuko cha Mto Rufiji, uvukaji wake unapata salaam kamili, mara pantoni mbovu, mara hiki na kile, inakula siku mbili. Pantoni hiyohiyo Feri Dar imeshatuachia majonzi, tena huduma zake mwisho saa sita usiku.



Abiria wa treni yenye mabehewa ya zamani, wakisubiri kupanda. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Tumshukuru mzee Benjamin William Mkapa, aliliona hilo, tena analijua fika njia ya nyumbani kwao pale Ikwiriri Rufiji, akajenga daraja linalojitosheleza, sijui wale wazaliwa wa miaka ya 1990 wanalijua hilo?

Unatoka hapo, unasonga hadi Nangurukulu, Kilwa kwa shida, ukianza tu uelekeo wa Lindi na mvua ikinyesha, imekula kwako, lazima mnase kwenye matope, kigezo na masharti kutoka hapo, ni jua kuwaka na tope kukauka. Wanaoishi vijiji jirani kama Mavuji, mkoani Lindi wanajua vizuri kilichoendelea hapo, leo hii ikibaki kuwa hadithi.

Naam, simulizi ni ile ile ndiyo umefika Masasi na kulala, asubuhi unaanza na mabasi kuelekea Tunduru, shughuli nzito kweli kweli. Maana nakumbuka kuna siku tulianza saa nne asubuhi, stendi ya Masasi nilikolala baada ya safari kutwa nzima kutoka Dar es Salaam, wakati leo hii anayetoka jiji hilo asubuhi anawahi kuona mechi ya soka alasiri mwanzo hadi mwisho, basi tukasonga huku mvua inanyesha kidogo yaliyotukuta ni mazito hasa, hadi kufika Tunduru stendi ilikuwa siku iliyofuata alfajiri.

Nilidiriki kukufuru kwa kujiuliza, ni Tanzania hii hii au kwingine? Maana nilipoangaza stendi zima yamejaa magari aina ya Land Rover tena aina ya 109. Wazaliwa wa 1990 mnayajua? Shughuli ikawa pevu vilevile wakati wa kuondoka, niliposema safari hiyo nipitie Tunduru hadi Namtumbo Songea, nako ikawa kutwa nzima, tena gari aina ya 'pick up', hadi nakuja kuiona Namtumbo Ruvuma, nguo zote zimejaa udongo mwekundu mithili ndiyo rangi yake ya asili.

Lakini maendeleo yakaja, Rais Kikwete, mnano Aprili 2006, nikamsikia ziarani Tunduru akiahidi kukomboa barabara yao kwa mradi maalum, kwani ilipita miaka mingi? Eti leo hii, basi linatoka Temeke Sudan mapema asubuhi, saa 9:00 alasiri linakatiza Masasi, usiku watu waangalia TV mjini Songea. Mbona raha!

Zama hizo hizo, waendao mkoa wa Mara kutoka Dar, sharti wakatize Arusha, kupitia nchini Kenya na alfajiri siku inayofuata wanaibukia Sirari Tarime kule kwa jamaa zetu, mchana wapo mjini Musoma. Waendao Bukoba nao kutoka Dar, njia hiyo hiyo wanapita Kenya hadi mpaka wa kuingia Uganda kuvuka hadi mpaka wa Mutukula kuja kuitafuta Bukoba mjini, kama siyo siku tatu ni nini hapo? We uliyopo Dar, ukifikiria kwenda nyumbani Bukoba, unawaza nauli, safari siku kadhaa na pasipoti juu.



Ndivyo yalivyo mabehewa mapya yaliyoingia nchini mwezi huu, yakiwa na huduma zote zenye stadi za kisasa.

Turejee kwenye safari za mabinamu zetu wale wa treni kwenda kuisaka Kigoma, Mwanza, Tabora na Mpanda. La kwanza kabisa, tenga siku mbili hadi tatu upaone uendako.

Sasa mabehewa yenyewe, siyo haya mnayoyajua nyinyi au kuyaona kwenye mitandao, labda kwa mbali ni kama yale yanayotumika daladala Dar es Salaam, au mabinamu zangu wanaosonga kwenda mwisho wa reli. Nikumegee kidogo, maana huwa sichoki kusimulia kipengele hiki kinanikumbusha mbali kweli kweli! Mpaka tiketi ipatikane abiria keshasota wiki mbili stesheni. Ukiingia kwenye mabehewa ya daraja la tatu unakutana na siti ambazo hazina sponji, feni na hata baadhi ya madirisha hayafungi.

Ukikuta juu kuna feni hilo litakuwa limeharibika. Sijajua kama yaliyokuwa yakiharibika ndiyo yanahamishwa daraja la tatu au vipi, lakini msamiati wa feni tu haukuwapo.Tofauti kubwa wa wakati ule wa daraja la kwanza la pili na la tatu ilikuwa ni idadi tu ya watu chumbani. La kwanza kulikuwa na wachache ambao wana uhuru wa kukaa bila bughudha, utaratibu wa kulala; la pili kukulikuwa na watu wengi kidogo kama sita hivi, angalau wakikaa kwa utulivu. Shughuli ilikuwa huko daraja la tatu.

Kwanza kulikuwa na mabehawa machache, hivyo abiria walikuwa wengi kiasi kwamba wengine siti hazikutosha, wakakalia mizigo yao, wengine chini ya sakafu, wapo waliokaa mpaka vyooni.

Kutokana na nyomi hiyo, wizi nao ulikuwa mkubwa wa mizigo, pia ilikuwa ngumu na jopo la watu kujishauri kwenda chooni hasa kinamama. Kusema kweli hadhi ya mabehewa na mazingira yalikuwa magumu, sijui enyi wa zama hizo mnajua?

Nikifikiria hapo, ndipo huwa napanda mashetani, mtu anapokosa mshipa wa aibu eti haoni maendeleo wala maboresho yoyote kwenye barabara, treni hata usafiri wa majini. Jamani, tema mate chini!

Mtu anaibuka waziwazi kwamba haoni tofauti kati ya karabai na taa ya umeme, au simu ya kiswaswadu na ya kupangusa kidole. Jamani, haya makubwa, mbona madogo yana nafuu!

*** Tuma meseji 0716 350534.**

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda yajibu shutuma za mataifa ya magharibi

**KIGALI, Rwanda**

RWANDA imeainisha "makosa" ya kushutumiwa kuwaunga mkono waasi wa M23 katika mzozo unaoendelea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Hali bado ni ya wasiwasi huku mapigano mapya kati ya jeshi na waasi wa M23 yakiripotiwa Alhamisi asubuhi karibu na mji wa Kitchanga huko Rutshuru, jimbo la Kivu Kaskazini mashariki mwa DRC.

Hivi karibuni, Ubelgiji ni taifa la magharibi ambalo liliiomba Rwanda "kusitisha msaada wote" kwa kundi la waasi la Watutsi wanaoongozwa na Watutsi wa Kongo baada ya Marekani, Ufaransa na Ujerumani, huku mashirika ya kutetea haki za Ulaya yakiomba EU kusitisha msaada wa kijeshi kwa Rwanda.

Katika barua iliyoandikwa kwa viongozi wa Umoja wa Ulaya, makundi hayo yalisema "kusimamishwa kwa shinikizo na misaada kwa Rwanda" na nchi za magharibi kulichangia kudidimiza mzozo huu mwaka 2012.

Katika taarifa, ili kukabiliana na shinikizo hilo, ikirejea mashambulizi ya makombora ya mwaka 2019 katika eneo lake, Rwanda ilisema ni "kosa kuchanganya" hatua za kulinda mpaka wake "kwa msaada wa kundi lolote lenye silaha nchini DRC".

"Kuilaumu Rwanda kunaonesha kutokuwa tayari kwa upande wa jumuiya ya kimataifa kukabiliana na vyanzo vya migogoro Mashariki mwa DRC", taarifa ya serikali inasema.

Rwanda pia ilisema mauaji ya hivi karibuni ya Kishishe dhidi ya raia, katika eneo linalodhibitiwa na M23, "yalitiwa hisia" na "uzushi wa serikali ya DRC" na kuongeza kuwa kuna dalili kuwa ni "makabiliano kati ya M23 na makundi haramu yenye silaha yanayoshirikiana na FARDC".




Wanajeshi wa Mali katika picha. **Picha: BBC.**

# Al Shabaab waua polisi wawili Kenya

**GARISSA, Kenya**

WAPIGANAJI wa Al Shabaab wameshambulia gari la polisi Mashariki mwa Kenya na kuwaua maofisa wawili na raia mmoja, polisi imesema.

Lori hilo lilikuwa likisafiri kutoka kambi ya Hayley Lapsset kuelekea mji wa Garissa, karibu kilomita 120 kutoka mpaka wa Somalia, wakati lilipogonga kifaa cha kulipuka, polisi walisema katika taarifa siku ya Jumatano.

Wanamgambo hao kisha walirusha guruneti kwa roketi kwenye gari hilo na kujihusisha na mapigano makali ya moto ambayo yalichukua maisha ya wahasiriwa, polisi walisema.

Redio ya Andalus ya Al Shabaab ilisema katika matangazo watu wenye silaha waliua maofisa wawili wa usalama wa Kenya na kuwajeruhi wengine kadhaa katika shambulio hilo.

Kundi hilo liliua watu 166 katika Chuo Kikuu cha Garissa mwaka 2015, na 67 katika maduka makubwa jijini Nairobi mwaka 2013, lakini mashambulizi ya mara kwa mara ya al Shabaab nchini Kenya yamepungua katika miaka ya hivi karibuni.

# Mali na Ivory Coast kutatua mivutano yao

**BAMAKO, Mali**

MALI inawashikilia wanajeshi 46 wa Ivory Coast iliowafungulia mashitaka ikiwatuhumu ni mamluki walioingia kwenye ardhi ya nchi yake.

Ujumbe wa Ivory Coast uliingia nchini Mali Alhamisi ukiongozwa na Tene Birahima Outtarra ambaye ametoa tamko kuhusu suala hilo la wanajeshi 46 wa nchi yake kushikiliwa na utawala wa Mali, akisema ni suala ambalo linatafutiwa ufumbuzi na wanachoweza kusema ni kwamba ziara yao nchini Mali imezaa matunda.

Birahima amesema ilikuweko hali ya kutoelewana baina ya jamhuri hizo mbili, Mali na Ivory Coast, miezi michache iliyopita na kwamba limekuwa jambo zuri wamekutana na kujadili.

Mvutano kati ya nchi hizo ulizuka Julai 10 pale wanajeshi 49 wa Ivory Coast walipokamatwa baada ya kuwasili katika uwanja wa ndege wa Mali, baadae watatu waliachiwa huru na 46 wakazuiliwa.

Wanajeshi hao wa Ivory Coast na Umoja wa Mataifa kimsingi walipelekwa Mali katika utaratibu wa kawaida wa kwenda kukisaidia kikosi cha Ujerumani ambacho ni sehemu ya ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa nchini Mali.

Lakini serikali mjini Bamako imetuhumu kwamba ni mamluki na mnamo mwezi Agosti walifunguliwa mashtaka ya kutaka kuuhujumu usalama wa nchi hiyo.

Taarifa ya makundi hayo imesema itashikilia msimamo huo mpaka utakapofanyika mkutano utakaosimamiwa na jumuiya ya Kimataifa na msuluhishi huru na utakaoamuwa kuhusu mustakabali wa makubaliano hayo.

# Bunge la Marekani latoa ripoti ya uvamizi

**NEWYORK, Marekani**

KAMATI ya Bunge la Marekani iliyokuwa inachunguza tukio la uvamizi katika majengo ya bunge la Marekani Januari 6, mwaka 2021 imechapisha ripoti ya mwisho ya uchunguzi huo.

Ripoti hiyo yenye kurasa 814 imeutaja uvamizi huo usiofikirika dhidi ya bunge hilo uliofanywa na wafuasi wa rais aliyeshindwa katika uchaguzi, Donald Trump.

Ripoti hiyo imetoa maelezo kuhusu juhudi za Trump kubatilisha uchaguzi wa rais wa 2020 na imetaja mapendekezo 11 kwa Bunge la Marekani na watendaji wengine kuzingatia ili kuimarisha taasisi za nchi hiyo dhidi ya majaribio ya matukio ya baadae kuhusu kuchochea uasi.

Miongoni mwa mapendekezo hayo ni kumzuia Trump kuwania tena urais. Kamati hiyo inatoa pia nakala kadhaa za maelezo ya mashahidi kutokana na mahojiano yake zaidi ya 1,000 na maelezo mapya ya kushangaza.

Wiki hii, kamati hiyo ilipendekeza rais huyo wa zamani afunguliwe mashtaka ya uhalifu.

# HABARI PICHANI



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Magila, Muheza mkoani Tanga, Shekhe Semtawa, akifungua mlango wa madarasa mapya mawili juzi, yaliyojengwa shuleni hapo pamoja na ofisi moja, ambavyo vyote ujenzi wake umekamilika na kuruhusu kudahili wanafunzi wa kidato cha kwanza, mapema mwakani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mwenyekiti wa Kijiji cha Magila wilayani Muheza, Tanga, Peter Mkwiji (wa kwanza kulia) akiwasimamia mafundi wa kuchimba mtaro kwa ajili ya ukarabati wa mabomba ya kupitisha maji baada ya kupasuka, na kusababisha baadhi ya mitaa kukosa huduma hiyo, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM.**




Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Salim Sechambo, akiwa amezungushiwa nyoka katika sherehe za maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara zilizofanyika uwanja wa Jitegemee, Muheza. Kulia aliyesimama ni msanii aliyefahamika kwa jina la Dokta Nyau. **PICHA: STEVEN WILLIAM.**




Wafagiaji wa barabara wakiwa kazini kwenye Barabara ya Morogoro, eneo la Magomeni Mapipa, Dar es Salaam juzi, bila kuweka alama inayoashiria kuwa wako kazini, kitendo ambacho kinaweza kusababisha ajali. **PICHA: SABATO KASIKA.**

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano imekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kiburi cha kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# Mtake Msitake-11

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

"Kwa maana hiyo pia ninaomba kiasi cha pesa kidogo ili nikawapelekee ndugu zake hapa kijijini kama rushwa wasiongeeongee sana. Halafu nataka nimlete kwako, ili umwambie kuwa wewe utagharamia matibabu yake yote mjini. Unajua tayari ameshaanza kuniuliza wewe pesa zote utatoa wapi? Nimemwambia nina wadau wangu watanisaidia."

"Yaani kwa plani yote uliyoifanya nakupa mia kwa mia, hata kesho mlete nimwambie mimi nitamgharamia kila kitu, safari pamoja na matibabu."

"Sawa ila subiri muda wa kumuondoa hapa utakuwa ule ambao nilikwambia tutaanza rasmi uhusiano. Miezi mitatu ijayo."

"Halafu tunampeleka Dar, Muhimbili tunamtelekeza."

"Sawa kabisa."

"Ila nina swali hapo kidogo Mary?"

"Lipi tena Usonzo na wewe?"

"Kama akitoka huko na kusema waliomtelekeza si anaweza kuja na polisi huku?"

"Sasa hapo tutakuwa wapenzi kamili kazi kwako baba."

"Basi nitakuhamisha hapa, nitakupeleka Arusha ukale kuku. Wakija hapa hola."

Walicheka pamoja na kugongesheana mikono.

"Na Enock je itakuwaje?" Lilikuwa ni swali la ghafla kutoka kwa Usonzo.

"Hilo niachie mimi. Kwani kanioa, ni mchumba tu? Na yeye ataachwa vile vile."

Kuna wakati Usonzo aliona kama anaota ndoto, msichana mrembo Mary aliyekuwa anamtoa udenda. Akamtongoza kwa njia zote, za kumlambisha asali na kutumia nguvu lakini zilidunda. Leo amemfuata mwenyewe ofisini na kila kitu kimeenda kama kilivyopangwa.

Alitaka kila kitu kitokee kwa muda mfupi ili awe ubavuni mwa mrembo huyo. Miezi mitatu aliiona ni mbali. Hata hivyo ilibidi kila kitu kiende kama kilivyopangwa na muda uliopangwa pia. Ilibidi tu awe mvumilivu.

******************************

Mwezi mmoja ulipita kiasi kwamba tukio lililotokea lilianza kusahaulika. Ingawa si kwa asilimia zote. Adel alibaki kwa kina Mary kama ilivyo makubaliano yao baada ya tukio hilo kutokea.




**"Samahanini sana, nimechelewa sana, unajua tena, unakwenda huko unakutana tena na watu wengine wenye shida zao."**

Lakini pia kwa mujibu wa Mary ni kwamba aliamua kuwa naye ili asiweze kushawishiwa na watu kwenda kushtaki.

Mzee Chale naye alikuwa ameshapewa mzigo wake wa rushwa na Usonzo kama alivyoombwa na Mary, akawa amelizima suala lile. Ikawa ni kama kosa la jinai kulizungumzia kijijini hapo. Likawa linanong'onwa tu. Kifupi sakata lilizimwa.

Siku ilifika ya Mary kumchukua na kumpeleka kwa Usonzo kwa ajili ya maandalizi ya safari ya kumpeleka kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ajili ya uchunguzi na matibabu zaidi.

Mary alimuongoza Adel akiwa ameshika mkono hadi kwenye ofisi za Usonzo. Walikaribishwa ofisini.

Ilikuwa ni mapema sana.

"Karibuni, ila nilikuwa natoka muda huu kwenda kunywa chai, sijui na nyinyi mnahitaji ili tuongozane?"

"Hapana sisi tumeshakunywa." Mary akajibu haraka haraka.

"Basi nitakuacheni hapa kwa muda kidogo, vumilieni tu jisikieni mko nyumbani, wewe Mary umeshapazoea."

"Ni kweli bosi." Mary akajibu.

Usonzo akanyanyuka na kumshika mkono Mary, akamvuta na kumkumbatia. Akambusu busu ambalo halikuwa na sauti.

Mary na Adel walikaa chumbani humo kwa kiasi cha saa nzima bila mwenyeji wao kurejea.

Akarejea baada ya saa moja na robo hivi.

"Samahanini sana, nimechelewa sana, unajua tena, unakwenda huko unakutana tena na watu wengine wenye shida zao."

"Hakuna wasiwasi 'faza'." Adel akajibu. Moja kwa moja Mosha Usonzo akaenda kuketi kwenye kiti chake cha ofisi.

Akamtazama Mary na kumkonyeza. Alikuwa na uhuru wa kufanya chochote kwa sababu Adel alikuwa haoni. Na hatoona licha ya kwamba wanajaribu kumtengenezea mazingira ya kwamba ataona tena wakimpeleka Muhimbili. Lakini lengo ni kumuondoa kijijini hapo kitaalam.

Mary alikuwa amevaa gauni yake fupi la bluu lililomfanya maeneo fulani ya mapaja kuwa wazi. Pia mabega yake yalikuwa wazi. Alivaa hivyo kwa makusudi ili kumtamanisha Usonzo atakachokiongea kisipingwe.

Kichwani alisuka nywele kwa mtindo wa rasta zenye mchanganyiko wa rangi nyeusi na udongo mwekundu. Alipendeza.

Akahamisha macho yake na kumtazama Adel Adam. Akatoa tabasamu la kejeli.

"Pole sana kijana."

"Anaitwa Adel bwana, kijana ndiyo nini?" Mary akadakia.

"Oooh, Adel."

"Ahsante sana bwana mwekezaji, nashukuru, na nimeshukuru sana leo kufika kwa mara ya kwanza kwenye ofisi zako, na kukusikia. Unajua mimi tena ndiyo sioni, ile nakusikia." Adel akajibu.

"Ooh, vizuri sana, nimependa kitu kimoja, wewe ni mtu wa Mungu sana, umeamua kumsamehe mtesi wako. Amekumwagia tindikali, lakini mmekaa mmeyaongea na kuamua kusameheana, hili ni jambo la kushukuru sana, unajua si wote wenye moyo huo." Akasema huku akitabasamu kwa dharau, akimtazama Mary.

Ukweli ni kwamba, Usonzo alionekana kumuonea huruma Adel kwa maneno, lakini machoni hakuonekana hivyo. Uso wake ulionekana kuwa wa kejeli na dharau. Na alifanya hivyo makusudi akijua Adel hawezi kujua kwa sababu haoni.

"Ni kweli bosi wangu kwa sababu vitabu vya Mungu vinasema samehe saba mara sabini. Mimi sina kinyongo, Mary ni rafiki yangu nilifahamiana naye siku chache tu tangu naingia kijiji hiki, lakini kilichotokea naona kama shetani tu alipita kati yetu." Akajibu bila kujua kuwa alikuwa anang'ong'wa.

"Sasa kijana ni hivi, mimi ndiyo niliyetoa pesa kwa ajili ya familia yako hapa kijijini, bibi yako na ndugu zako wengine. Leo pia nitakupa kiasi cha shilingi milioni moja kama pole, mwezi mmoja na nusu hivi ujao tumepanga mimi na Mary kukupeleka Muhimbili kwa ajili ya matibabu zaidi. Kwa mujibu wa madaktari ni kwamba unaweza kuona tena kama utapelekwa kwenye hospitali zenye vipimo vya kisasa. Kwa hiyo utaondoka hapa ukiambatana na mimi pamoja na Mary, sawa?"

"Nitashukuru sana bosi wangu, na ndiyo maana naendelea kuamini kuwa Mary alipitiwa na kitu ambacho si cha kawaida kufanya tukio hili, haikuwa dhamira yake ya dhati. Mimi binafsi kabla ya kufika hapa nimeongea na Mary na nimekubaliana nalo hilo. Nitakwenda kwenye matibabu na naamini naweza kuona tena."

Kwa sababu mhusika tayari alikuwa ameshakubaliana na kila kitu, hakukuwa na cha ziada na kwa sababu ameshakaa muda mrefu, Mary na Adel wakamuaga Usonzo, mfadhili wa safari na matibabu.

Walitoka mlangoni, lakini ni kama kuna kitu alisahau, akamwambia Adel asimame. Akarejea ndani na kuteta.

"Haya sasa kila kitu kimekamilika, kazi kwako."

"Yaani mimi nilivyofurahi Mary sikwambii kitu. Nataka nikuchukue moja moja moja uwe mke wangu."

"Mimi huyo?"

"Nani mwingine?"

"Haya baba uamuzi ni wako, kuchemsha, kukaanga au kula chukuchuku."

ITAENDELEA JUMAMOSI

# TFF YAKUNWA NA VIWANGO LIGI YA WANAWAKE

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania TFF limesema limefurahishwa na mwenendo wa Ligi Kuu ya Wanawake kwa viwango vilivyoonyeshwa na timu za Simba Qeens pamoja na Yanga Princess.

Katibu mkuu wa TFF, Wilfred Kidau amesema hamasa ya Ligi ya Wanawake msimu huu imekuwa kubwa tofauti na msimu uliopita.

"Hamasa msimu huu imekuwa kubwa nimefarijika kuona idadi kubwa ya mashabiki wamejitokeza kwa wingi kushuhudia mtanange huu, kitu ambacho hapo nyuma hakikuwepo," alisema Kidau.

Katibu huyo alisema timu hizo zimejiimarisha kwa kiasi kikubwa kutokana na usajili mzuri uliofanywa na mabenchi yao ya ufundi.

Alisema Ligi ya wanawake kwa sasa inazidi kushika kasi kwani hata zile timu ambazo hazikufanya vizuri msimu uliopita zinaonyesha ushindani mkubwa.

Alisema hiyo imetokana na kuwepo kwa walimu wenye ubora wa hali ya juu katika kufundisha soka la wanawake ikiwa ni pamoja na michezo yao kurushwa kwenye televisheni mbali mbali nchini.



Wasanii wa kikundi cha ngoma za asili kiitwacho Dumange cha mjini Korogwe mkoani Tanga, kikitoa burudani wakati wa mapokezi ya Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake CCM (UWT) Taifa, Mary Chatanda alipowasili mjini humo wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

## BMT yatangaza uchaguzi ngumi za wazi

**Na Shufaa Lyimo**

BARAZA la Michezo Tanzania (BMT) limetangaza uchaguzi wa viongozi wa Shirikisho la Ngumi za wazi Tanzania (OBFT) unaotarajiwa kufanyika Februari 12 mwakani jijini Dar es Salaam.

Akitangaza uchaguzi huo jana Kaimu Mkuu wa kitengo cha Uhusiano na Mwasiliano, Najaha Bakari alisema usaili wa wagombea kwa nafasi tofauti utafanyika Februari 10.

Alisema fomu zitaanza kutolewa kuanzia Januari 6 hadi 7.

Alitaja nafasi zinazogombewa kuwa ni Rais, Makamu wa Rais, Katibu Mkuu, Katibu Mkuu msaidizi, Mweka hazina, Mjumbe wa Kamati ya walimu, Mjumbe wa Kamati ya ufundi na Mjumbe wa Kamati ya mashindano na vifaa.

Pamoja na Mjumbe wa Kamati ya Wanawake na vijana, Mjumbe wa Kamati ya maendeleo ya Mikoa na Taasisi za Umma, Mjumbe wa Kamati ya mipango na fedha, mjumbe wa Kamati ya afya pamoja na mjumbe wa Kamati ya AOB, APB na WSB.

Kaimu huyo alitaja sifa za wagombea kwa upande wa nafasi ya Rais na Katibu mkuu kuwa awe raia wa Tanzania, awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea na awe amewahi kuongoza Chama au Taasisi yoyote ya Umma.

Alisema ahakikishe amethibitishwa na Kamati ya uchaguzi wa Shirikisho hilo na kudai awe na ujuzi wa mchezo huo,ambaye hajawahi kuucheza na kuongoza katika nyanja yoyote.

Alisema wagombea wote wanatakiwa wahakikishe wanafahamu vizuri Katiba ya OBFT, ikiwamo Katibu mkuu na makamu wake waweze kutumia kompyuta katika matumizi ya kawaida na uzoefu wa uongozi.

Aidha alisema Mweka hazina awe na elimu ya uhasibu kuanzia ngazi ya cheti pamoja na sifa zote zilizotajwa.

Kwa upande wa Wajumbe awe mtanzania, ajue kusoma na kuandika,hana kosa la jinai,awe hajaongoza Shirikisho kwenye nafasi za juu,awe ameucheza huu mchezo ikiwemo kuzifahamu sheria zake.

Kamati ya walimu mgombea anatakiwa awe na cheti cha ualimu wa mchezo huo katika ngazi yoyote.

"Kwa upande wa Kamati ya wanawake mgombea awe mwanamke ambaye alishawahi kuongoza chama au Taasisi yoyote mwenye elimu ya kuanzia kidato cha nne na ahakikishe anaielewa Katiba vizuri, alisema.

## Kocha Simba Queens asema ligi ni ngumu

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukulu amesema Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ya msimu ina ushindani mkubwa na kila timu imejipanga kupambania ubingwa.

Lukulu amekiongoza kikosi cha Simba katika mechi tatu za ligi ikiwemo dhidi ya Yanga Princess mchezo uliopigwa uwanja wa Benjamin Mkapa na kumalizika kwa sare ya 1-1.

Akizungumza na gazeti hili hili Kocha huyo alisema timu zimefanya maandalizi mazuri na kila moja inajiandaa vizuri ikikutana na Simba Queens.

Alisema kuhusu mchezo wao na Yanga ulikuwa mgumu na wenye upinzani, kama wangetumia vizuri nafasi walizopata wangeondoka na pointi zote tatu.

"Ni kweli ligi ni ngumu, kila timu imejipanga vizuri ushindani ni mkubwa na umeanza mwanzoni kwa hiyo tunapaswa kujipanga, unajua tumecheza Ligi ya Mabingwa Afrika na ndiyo Mabingwa watetezi kwa hiyo kila timu ikikutana nasi inapambana vilivyo," alisema kocha huyo.

Alisema wamelazimika kufanya mabadiliko ya kikosi kwa kuwaweka benchi baadhi ya wachezaji ambao wamewahi kunolewa na mpinzani wake, Sebastian Nkoma kwa sababu anawafahamu vizuri.

"Nimemuweka benchi Vivian Corazone Asha Djafar na Olaiya Barakat kwa sababu nawafahamu vizuri amewahi kuwafundisha ningeanza nao basi mechi ingekuwa ngumu kwa upande wetu na wao kuingia katika kipindi cha pili na kupata matokeo .

Kipindi cha pili tulilazimika kubadilisha mbinu na kucheza mipira mirefu kwa sababu tuliona Yanga wamechoka na mabadiliko tuliyoyafanya imetusaidia na kuondoka na pointi moja," alisema Lukulu.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nkoma alisema mchezo ulikuwa mgumu na ushindani mkubwa licha ya kushindwa kutumia vizuri nafasi wachezaji wake wamepambana na kupata pointi mmoja.

Alisema katika mchezo huo wa juzi alikuwa akitafuta mambo mawili sare au ushindi mbele ya timu bora, Simba Queens na kufanikiwa kuondoka na alama moja na anaimani baada ya muda timu yake itakuwa na muunganiko mzuri .

"Tunashukuru Mungu tumepata alama 1 siyo mbaya mchezo ulikuwa mzuri kwa upande wetu. Nafurahi kuona wachezaji wangu wameanza kujiamini kwenye mechi kama hizi za dabi, hiyo Simba queens ambayo unaiona leo mimi ndio nilietengeneza hiyo timu sasa jiulize nikipata muda wa miezi 3 tu Yanga Princess hii itakuajе," Nkoma.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM AITA REAL MADRID

KIUNGO wa kati wa England, Jude Bellingham anapendelea kujiunga na Real Madrid kutoka Borussia Dortmund, licha ya Liverpool, Manchester City na Manchester United kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(AS)***

### FERNANDEZ BEI KUBWA

KLABU ya Benfica imekataa ofa ya euro milioni 100 kutoka kwa klabu ambayo haijatajwa jina kwa ajili ya kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool na Real Madrid, na haitamuuza kwa chini ya euro milioni 120 mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 (£106m)**.** ***(Record)***

### LOCATELLI AWINDWA

REAl Real Madrid wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Italia, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 24 ambaye yuko kwa mkopo Juventus kutoka Sassuolo, ikiwa watamkosa Jude Bellingham au Enzo Fernandez. ***(AS)***

### FOFANA KUTUA CHELSEA

CHELSEA imefikia mkataba wa euro milioni 12 na Molde ili kumsaini mshambuliaji wa Ivory Coast, David Datro Fofana mwenye umri wa miaka 20. (Fabrizio Romano)

### MENDY AKATAA

GOLIKIPA wa Chelsea na Senegal, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 30, amepuuzilia mbali mkataba mpya wa miaka sita pale Stamford Bridge kwa sababu anaamini kuwa klabu hiyo haimuoneshi "heshima" ya kutosha linapokuja suala la mshahara. ***(Sun)***

### MUDRYK KUTUA ARSENAL

MTENDAJI Mkuu WA Shakhtar Donetsk, Carlo Nicolini amethibitisha kuwa Arsenal ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Ukraine, Mykhailo Mudryk mwenye umri wa miaka 21. ***(Calciomercato)***

### RABIOT NAYE AWINDWA

ARSENAL inajaribu kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake utamalizika Juventus msimu wa joto. ***(Repubblica, via Mail)***

### SOARES HAJARUHUSIWA

ARSENAL bado hawajaamua iwapo watamruhusu mlinzi wa Ureno, Cedric Soares kuondoka Januari, huku Fulham wakiongoza mbio za kumsaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ambaye pia anawavutia Bayer Leverkusen na Villarreal. ***(Evening Standard)***

### BASTONI ATAKIWA

INTER Milan inameanza mazungumzo ya mkataba mpya na beki wa Italia, Alessandro Bastoni kuhusu mkataba mpya, huku Manchester City na Tottenham zikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(La Gazzetta Dello Sport)***

### DE PAUL NUSURA ATUE LEEDS

KIUNGO wa kati wa Argentina, Rodrigo De Paul mwenye umri wa miaka 28, alikaribia kujiunga na Leeds United kutoka Udinese kabla ya kuhamia Atletico Madrid. ***(TalkSPORT)***

### DIAZ KUBAKI

MSHAMBULIAJI wa Blackburn na Chile, Ben Brereton Diaz mwenye umri wa miaka 23 huenda akasalia Ewood Park Januari hii na kuweka chaguo lake wazi kwa uhamisho wa bila malipo msimu wa joto. ***(Football League World)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BARCELONA YAPANGA KUMREJESHA MESSI

**Rais asema wanapambana kuhakikisha anarudi kwenye himaya yao na...**

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amesema nia yao kubwa ni kutaka Lionel Messi arejee katika klabu hiyo.

Barca ilimleta Messi Ulaya akiwa mdogo, na alijiimarisha kama gwiji wa Blaugrana hao na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa klabu hiyo na kushinda Ballons d'Or saba akiwa Camp Nou.

Messi pia aliisaidia Barca kushinda mataji 10 ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, na mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati akiwa hapo Katalunya, katika kipindi ambacho kilikuwa ni kimojawapo cha mafanikio zaidi katika klabu hiyo.

Hata hivyo, matatizo ya kifedha yalimaanisha kuwa wababe hao wa LaLiga hawakumuongezea Messi mkataba wake ulipoisha mwaka 2021, na Paris Saint-Germain waka-harakisha kumsajili katika mji mkuu wa Ufaransa kwa mkataba wa miaka miwili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 alitwaa Kombe la Dunia akiwa na Argentina kwa mara ya kwanza wikendi iliyopita.

Huku Messi akionesha kuwa bado anaweza kucheza kwa kiwango cha juu sana, kuna mjadala juu ya mustakabali wake na mkataba wake wa PSG unafikia tamati Juni 2023.

Inasemekana PSG walikuwa na makubaliano ya mdomo ya kuongeza mkataba wake, lakini Laporta hakuficha nia yake ya kutaka kumrejesha fowadi huyo kwenye klabu hiyo.

"Ni dhahiri kwamba ningependa arudi siku moja," alisema Laporta akiiambia BarcaTV. "Ningependa, lakini hatuwezi kutoa matarajio.

"Tungependa sana arudi, lakini ni jambo ambalo itabidi tuone."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,059,8

MECHI KALI
RUVU SHOOTING
VERSUS
NAMUNGO
1 | 3.40
X | 2.77
2 | 2.25

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARTETA APANGA KUIBORESHA ARSENAL

**LONDON, England**

ARSENAL inatafuta mchezaji wa kuwapeleka katika "kiwango kinachofuata" katika dirisha la usajili la Januari baada ya kumpoteza Gabriel Jesus kutokana na jeraha, kwa mujibu wa kocha, Mikel Arteta.

Washikabunduki waliingia kwenye mapumziko ya Kombe la Dunia wakiwa na pointi tano mbele ya mabingwa Manchester City kwenye kilele cha Ligi Kuu ya England.

Jesus amekuwa na mchango mkubwa Arsenal msimu huu, lakini alifanyiwa upasuaji mapema mwezi huu baada ya kuumia goti wakati wa kampeni ya Kombe la Dunia Brazil.

Huku ripoti zikisema kwamba Jesus anaweza kuwa nje kwa miezi mitatu, Arteta analenga nyongeza - ingawa atahamia tu kwa mchezaji anayefaa.

"Sijawahi kutoa tarehe kuhusu Jesus - itachukua muda, kwa hakika. Amefanyiwa upasuaji," alisema Arteta katika mkutano na waandishi wa habari.

"Lazima tuwe na bidii, tunatafuta kuimarisha timu. Lazima awe mchezaji sahihi. Tunahitaji mchezaji ambaye atakuwa na athari na kutupeleka kwenye kiwango cha juu.

"Tunajua tulipo katika suala la kikosi na namba. Tutakuwa waangalifu sana kuhusu kile tunachotaka kufanya kwenye dirisha."

Arteta pia alifichua kuwa aliwasiliana ana kwa ana na uongozi wa klabu wakati wa mapumziko ya Kombe la Dunia, ili kupanga kile ambacho kinaweza kuwa nusu ya pili ya msimu.

"Sisi daima tunaunganishwa, na uhusiano huo unazidi kuwa na nguvu zaidi. Ni uhusiano wa pekee sana hivi sasa," alisema.

# Ten Hag hataki Wan-Bissaka aondoke Man

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag alitoa jibu lisiloeleweka alipoulizwa ni lini Jadon Sancho atarejea Manchester United, lakini akasisitiza Aaron Wan-Bissaka ana mustakabali katika klabu hiyo.

Sancho aliichezea United mara ya mwisho Oktoba 22 katika sare ya 1-1 dhidi ya Chelsea na aliondolewa kwenye kikosi cha England kilichoshiriki Kombe la Dunia.

Winga huyo hakusafiri na kikosi kwa ajili ya kambi ya mazoezi ya hali ya hewa ya joto nchini Hispania badala yake aliwekwa kwenye programu ya kibinafsi kufanyia mazoezi ya utimamu wake.

United walirejea uwanjani Jumatano katika ushindi wa 2-0 dhidi ya Burnley kwenye Kombe la EFL na kocha Ten Hag aliulizwa kama anajua ni lini Sancho angepatikana ambapo alijibu tu: "Hapana."



Akibanwa ikiwa kuna ratiba ya kurejea uwanjani kwa nyota huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, Ten Hag alitoa jibu lile lile.

Hata hivyo, alitoa jibu refu zaidi kwa maswali kuhusu Wan-Bissaka, ambaye amekuwa na majeraha msimu huu.

Beki huyo wa pembeni alimtengenezea Christian Eriksen bao la kwanza la United, kabla ya kazi nzuri ya Marcus Rashford kuiwezesha United kutinga hatua ya nane bora.

Wan-Bissaka amekuwa na matatizo ya kuwa na uthabiti tangu alipowasili kutoka Crystal Palace mwaka wa 2019 na amekuwa akihusishwa na kuondoka klabuni hapo.

"Aaron Wan-Bissaka, ni wazi ana mustakabali," alisema Ten Hag akiwaambia wanahabari siku ya Jumatano.

"Amekuwa na miaka mizuri na United, lakini tangu mwanzoni mwa msimu huu alikuwa na majeraha."

344,733/-

# TANGWA PEPETA SASA HAKUNA KULALA

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya Tangwa Pepeta imesema baada ya uzinduzi wa albamu ya 15, hakuna kulala, badala yake itaendelea na maonyesho kama kawaida.

Uzinduzi wa albamu hiyo iitwayo Chombo ya Fundi, ulizinduliwa wiki iliyopita katika ukumbi wa Gwambina Lounge, Chang'ombe Dar es Salaam.

Meneja wa bendi hiyo, Hassan Rehan, alisema miaka ya nyuma Tangwa Pepeta ilikuwa ikizindua albamu kisha wanamuziki wanapumzika siku moja.

"Kwa sasa maisha yamebadilika, hatuwezi kuendelea kufanya kazi kwa mazoea, hivyo baada ya uzinduzi tutaendelea na kazi kama kawaida," alisema Rehan.

Alifafanua kuwa bendi hiyo ilitoa burudani eneo la Mtoni Kijichi siku moja baada ya kumaliza uzinduzi.

"Hii ni Tangwa Pepeta forever, hivyo mambo yetu yanakwenda na wakati, ili kuhakikisha mashabiki wetu wanapata kile wanachotaka," alisema.

Bendi hiyo ilianzishwa mwaka 1998 na imetoa albamu 14 zilizochangia kupa umaarufu, na sasa imezindua ya 15.

Baadhi ya albamu hizo ni "Jirani" iliyotoka mwaka 2000, "Chuki Binafsi" 2002, "Password" mwaka 2006, "Mtaa wa Kwanza" mwaka 2008, "Usiyaogope Maisha" 2015 na sasa Chombo ya Fundi" mwaka 2022.




Wanamuziki wa bendi ya Twanga Pepeta wakifanya vitu vyao kwenye uzinduzi wa albamu ya 15 ya 'Chombo ya Fundi', jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# YANGA, AZAM FC MECHI YA KIBABE

INATOKA UK. 32

na wamerejea tayari kwa ajili ya kuwavaa Yanga.

Alisema anatambua ni mchezo wa ushindani mkubwa kwa sababu wao wanahitaji kuendelea kutafuta pointi muhimu pamoja na Yanga wakihitaji matokeo ili kujihakikisha kukaa kileleni.

"Maandalizi yetu yako vizuri na tuko tayari kwa mchezo wetu huo, utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji kufikia malengo, tunawaheshimu Yanga na tutaonyesha mchezo mzuri," alisema Kocha huyo.

# Simba yaja juu

INATOKA UK. 32

sipate pointi tatu, kwa hiyo wameahidi kupambana ili kurejesha furaha," alisema.

Kwa sasa Simba inakamata nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi moja tu zaidi dhidi ya Azam FC inayoshika nafasi ya tatu na sita dhidi ya anayeongoza.

Ina pointi 38, Azam FC ikiwa na 37, Yanga iko kileleni ikiwa na pointi 44.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/22 | 18:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/12/22 | 18:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 03. 26/12/22 | 18:00 | Rotherham United vs Stoke City | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 04. 26/12/22 | 18:00 | Burton Albion vs Lincoln City | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 05. 26/12/22 | 18:00 | Cambridge United vs Shrewsbury Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 26/12/22 | 18:00 | Charlton Athletic vs Peterborough United | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 26/12/22 | 18:00 | Exeter City vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.55 |
| 08. 26/12/22 | 19:00 | FC Annecy vs AS Saint-Etienne | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 09. 26/12/22 | 20:00 | Goztepe Izmir vs BB Bodrumspor | 2.50 | 3.35 | 2.65 |
| 10. 26/12/22 | 20:15 | Cardiff City vs Queens Park Rangers | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 26/12/22 | 22:45 | Royal Charleroi SC vs RSC Anderlecht | 2.80 | 3.45 | 2.38 |
| 12. 26/12/22 | 22:45 | Luton Town vs Norwich City | 2.75 | 3.30 | 2.50 |
| 13. 26/12/22 | 23:00 | Valenciennes FC vs Amiens SC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 14. 26/12/22 | 23:00 | Pau FC vs Paris FC | 2.95 | 3.20 | 2.38 |
| 15. 26/12/22 | 23:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs Grenoble Foot | 2.46 | 3.05 | 2.95 |
| 16. 26/12/22 | 23:00 | SC Bastia vs SM Caen | 3.05 | 3.10 | 2.38 |
| 17. 26/12/22 | 23:00 | Nimes Olympique vs EA Guingamp | 2.90 | 3.25 | 2.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 24/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3825 | Singapore vs Myanmar | 1.41 | 4.39 | 6.05 |
| 13:30 | 5406 | Hatayspor vs Giresunspor | 2.06 | 3.58 | 3.23 |
| 13:30 | 5428 | Havadar vs Nassaji Mazandaran | 2.83 | 2.59 | 2.78 |
| 13:30 | 5507 | Tuzlaspor vs Altay | 2.20 | 3.26 | 2.96 |
| 14:00 | 4918 | Persik Kediri vs Persis Solo | 3.40 | 2.95 | 2.28 |
| 14:00 | 5496 | Ihefu FC vs Mtibwa Sugar | 2.39 | 2.82 | 3.06 |
| 14:00 | 5907 | PS Tni vs Persib Bandung | 4.58 | 3.31 | 1.72 |
| 14:30 | 2949 | Aluminium Arak vs Gol Gohar | 2.91 | 2.53 | 2.77 |
| 14:30 | 3936 | Sepahan Esfahan vs Naft Masjed Soleyman FC | 1.37 | 4.07 | 8.14 |
| 15:00 | 3006 | Mumbai City FC vs Chennaiyin FC | 1.40 | 4.67 | 5.83 |
| 15:30 | 2614 | St Mirren vs Aberdeen | 2.79 | 3.18 | 2.49 |
| 15:30 | 5083 | Celtic vs St Johnstone | 1.11 | 8.14 | 18.87 |
| 15:30 | 5282 | Malaysia vs Laos | 1.03 | 10.69 | 28.18 |
| 15:45 | 1446 | Aswan vs Enppi Club | 2.54 | 3.04 | 2.84 |
| 15:45 | 1914 | Al Nasr Dubai vs AL Bataeh (UAE) | 1.40 | 4.47 | 6.21 |
| 15:45 | 2279 | Baynounah vs AL Tawon SC | 3.88 | 3.79 | 1.73 |
| 15:45 | 4606 | AL Urooba vs AL-Rams | 1.88 | 3.98 | 3.15 |
| 15:45 | 4937 | Dubba Al-Husun vs Al-Hamriyah | 1.60 | 3.99 | 4.48 |
| 15:45 | 5026 | Jazira Abu Dhabi vs Al Dhafra | 1.14 | 6.79 | 12.61 |
| 16:00 | 1616 | Ruvu Shooting vs Namungo | 3.40 | 2.77 | 2.25 |
| 16:00 | 1953 | Dumbarton vs East Fife | 1.85 | 3.60 | 3.55 |
| 16:00 | 3221 | Kasimpasa vs Sivasspor | 2.23 | 3.43 | 2.98 |
| 16:00 | 3253 | Denizlispor vs Yeni Malatyaspor | 2.64 | 3.28 | 2.40 |
| 16:00 | 4127 | Kelty Hearts FC vs Dunfermline | 3.16 | 3.50 | 2.07 |
| 16:00 | 4157 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Hadera | 1.18 | 6.04 | 11.68 |
| 16:30 | 1657 | El Bayadh vs MC Alger | 2.47 | 2.72 | 3.05 |
| 16:30 | 2085 | MES Rafsanjan vs Malavan Bandar Anzali | 1.75 | 3.02 | 5.06 |
| 16:30 | 2407 | USM Khenchela vs ASO Chlef | 1.67 | 3.30 | 5.05 |
| 16:30 | 3571 | USM Alger vs CS Constantine | 1.91 | 3.06 | 3.98 |
| 16:30 | 4340 | Foolad Khuzestan vs Zob Ahan | 2.11 | 2.67 | 3.98 |
| 16:30 | 5780 | HB Chelghoum Laid vs MC Magra | 6.42 | 3.79 | 1.47 |
| 16:30 | 5962 | Paradou AC vs RC Arbaa | 1.91 | 3.06 | 3.98 |
| 17:00 | 3261 | Hibernian vs Livingston | 1.83 | 3.44 | 4.19 |
| 17:00 | 3262 | MC Oran vs US Biskra | 2.02 | 2.92 | 3.80 |
| 17:00 | 3744 | Dundee Utd vs Hearts | 2.93 | 3.43 | 2.26 |
| 17:00 | 4603 | Edinburgh City vs Peterhead | 1.43 | 4.43 | 6.30 |
| 17:00 | 5268 | Northeast United FC vs ATK Mohun Bagan | 5.64 | 4.38 | 1.44 |
| 18:00 | 1255 | JS Kabylie vs CR Belouizdad | 2.91 | 2.72 | 2.57 |
| 18:00 | 4057 | Haras EL Hodood vs National Bank | 3.18 | 2.68 | 2.58 |
| 18:00 | 4537 | Ghazl EL Mahallah vs Farco FC | 2.38 | 2.64 | 3.63 |
| 18:30 | 3099 | Al Ain vs Al Wasl Dubai | 1.56 | 4.18 | 4.57 |
| 18:30 | 5465 | Hapoel Katamon vs Ironi Kiryat Shmona | 2.13 | 3.12 | 3.22 |
| 19:00 | 3072 | Pendikspor vs Manisa BBSK | 1.98 | 3.36 | 3.36 |
| 19:00 | 5470 | Sectzya Nes Ziona vs FC Ashdod | 3.12 | 3.36 | 2.08 |
| 19:00 | 5873 | Trabzonspor vs Fenerbahce | 2.72 | 3.37 | 2.44 |
| 19:00 | 5913 | Hapoel Haifa vs Maccabi Bney Reine | 2.05 | 3.07 | 3.51 |
| 20:00 | 3245 | Coca Cola vs Talaea El Gaish | 1.78 | 3.28 | 4.78 |
| 20:00 | 4216 | ES Setif vs JS Saoura | 1.94 | 3.06 | 3.88 |
| 20:30 | 5971 | Hapoel Beer Sheva vs Beitar Jerusalem | 1.44 | 4.30 | 5.86 |
| 20:45 | 1910 | Societe Omnisport vs Bassam | 1.89 | 3.25 | 4.30 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Desemba 24, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Barcelona yapanga kumrejesha Messi



Wachezaji wa Yanga, Salum Abubakar 'Sure Boy' akiwa na Yannick Bangala kwenye mazoezi. **PICHA: YANGA**

# YANGA, AZAM FC MECHI YA KIBABE

●●●Zote zabadili jezi za nyumbani huku Nabi akisema...

**Na Saada Akida**

AZAM FC imeamua kuja kivingine kwa kubadili jezi zao za nyumbani kwa kutumia za ugenini katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho Jumapili.

Azam wamefuata nyayo za Yanga ambao wameamua kutumia jezi nyeusi badala ya njano katika michezo yake ya nyumbani.

Miamba hiyo inashuka uwanjani huku kila moja akiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 2-2 mchezo wa raundi ya kwanza uliochezwa kwenye Uwanja wa Mkapa.

Yanga inashuka kumenyana na Azam ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara kwa pointi zake 44 ikifuatiwa na Simba yenye alama 38.

Kuelekea mchezo huo Yanga iliingia kambini juzi huku Azam wakiweka kambi ya siku tatu Mwanza na imerejea rasmi kwa ajili ya mchezo huo kuhakikisha wanavuna pointi mbele ya wanaongoza ligi hiyo.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amesema mchezo wao na Azam ni wa ushindani mkubwa na wanatakiwa kuwa makini kwenye maandalizi yao.

Alisema wako makini katika maandalizi yao kwa sababu ya ubora wa wapinzani wao na uwepo wa wachezaji ambao wanaweza kuwapa matokeo.

"Hii ni mechi muhimu kwa kila timu kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji pointi, kwa upande wetu tuko makini na maandalizi yetu kufanyia kazi madhaifu ya kikosi chetu," alisema Nabi.

Alisema wanatambua ubora na uimara wa Azam kwa kuangalia baadhi ya mechi zao, kwa kuhakikisha wanaingia kwa mbinu tofauti na michezo iliyopita ya ligi hiyo.

Kocha wa Azam, Kali Ongala alisema baada ya mchezo wao na Geita Gold FC, waliweka kambi ya siku tatu jijini Mwanza

INAENDELEA UK. 31

## Simba yaja juu Phiri kuumizwa

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imekuja juu na kuwataka waamuzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa makini na baadhi ya wachezaji ambao badala ya kucheza soka kazi yao ni kuumiza wenzao kwa makusudi.

Klabu hiyo imesema hayo baada ya kuumizwa straika wake tegemeo Mosses Phiri kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera na kutoka sare ya bao 1-1.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo amesema jana kuwa kwa sasa Phiri hawezi kukanyaga chini na anatembea kwa kutumia gongo, ingawa ni mapema kusema kama atacheza au hatocheza mechi ijayo dhidi ya KMC Jumatatu ijayo.

"Phiri aliumizwa kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar, kwa upande wetu tunaona kama ni mchezo wa hovyo, wa kihuni, kila alipokuwa anagusa mpira alikuwa anachezewa rafu mbaya kwelikweli, wakafanikiwa kumuumiza akatoka nje, amefanyiwa vipimo majibu bado ili tuweze kujua ni kiasi gani ameumia na atakaa nje kwa muda gani, chochote kitakachotamkwa tunawajulisha Wanasimba juu ya hali ya mchezaji Phiri, lakini nitumie fursa hii kuwaomba wachezaji wa ligi ya Tanzania kama mpira unavyojieleza cha kwanza ni kulinda afya yako na ya mchezaji mwenzako, hii ni kazi kwa hiyo unapomchezea mwenzako vibaya, maana yake ni kwamba unahatarisha kazi yake kwa hiyo inakuwa haileti picha nzuri. Tuchezeane mpira wa nguvu, lakini siyo mpira wa kuumizana kwa sababu unaharibu ndoto na maisha ya mtu. Lakini vile vile kwa waamuzi wajitahidi kuziona na kuzichukulia hatua rafu za mara kwa mara kwa mtu huyo mmoja, wajitahidi kuchukua hatua stahiki ili kila mmoja apate haki yake uwanjani," alisema Ahmed.

Kwa siku za karibuni kumekuwa na aina za rafu mbaya kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu ambazo zinahatarisha karia za wachezaji wenyewe.

Wakati huo huo, Ahmed alisema wamejipanga vema kwenye mchezo wao dhidi ya KMC, ambapo wachezaji wameahidi. kutowaangusha mashabiki wao, hivyo wameahidi kupambana ili kuwarejeshea furaha.

"Hatukupata ushindi kwenye mechi iliyopita, wachezaji wanalijua hilo, haiwezekani tena kwa mara ya pili tu-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042